# *Uinjilisti Wa Wakati Wa Mwisho*

Asante, Ndugu Orman.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu sasa kwa ajili ya maombi. Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, sijui kama kuna yeyote hapa angekuwa na haja maalum angetaka ijulikane kwa mkono ulioinuliwa? Bwana anaona mambo haya, nina hakika. Nikitumaini atayajalia.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tumekusanyika asubuhi ya leo si kwa kusudi lingine ila kulitukuza Jina la Bwana wetu Yesu. Nasi tunakushukuru Wewe ya kwamba tayari tumeuhisi Uwepo Wake. Nasi tuna hakika ya kwamba Yeye hukutana nasi, kwa sababu ni ahadi Yake, kwamba "Popote wawili ama zaidi wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa miongoni mwao." Sasa, tungeomba baraka Zako, Bwana, juu ya haja hizi zote leo hii ambazo zimejulikana sasa kwa kuinuliwa kwa mikono. Unajua kilichokuwa chini ya mkono huo, moyoni, nami naomba kwamba utamjibu kila mmoja.

3 Tunakushukuru Wewe leo hii kwa ajili ya nafasi ya kukuabudu. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya kanisa na kwa ajili ya watu na kwa ajili ya ndugu wa Imani moja na sisi yenye thamani. Na sasa tunaomba ya kwamba Wewe utatupatia shauku za moyo wetu leo, hiyo ni, kukutumikia Wewe. Tulishe kwa hiyo Mana iliyofichwa uliyosema, katika Biblia, iliyotolewa, iliyowekwa akiba kwa ukuhani pekee. Nasi tumefundishwa ya kwamba sisi ni makuhani wa Mungu, tukitoa dhabihu ya kiroho, hiyo ni, matunda ya midomo yetu, tukilisifu Jina Lake. Sasa, tunaomba ya kwamba utatubariki katika sehemu ijayo ya ibada hii, kutumegea Mkate wa Uzima. Katika Jina la Yesu. Amina.

4 Nina furaha kuona familia yetu kubwa imerudi tena asubuhi ya leo, nami nina furaha kuwa hapa pamoja nanyi. Na, pia, wageni wanaokaa sehemu mbalimbali za nchi, wanaokusanyika pamoja nasi Jumapili asubuhi, wako hapa. Sisi hatuna dhehebu. Nasi tunakusanyika tu, watu wanaomwamini Mungu wanakusanyika pamoja kumwabudu Bwana pamoja, na kufanya maombi yetu kwa Mungu, kufanya maungamo yetu Kwake. Na kila Jumapili na kila siku tunapitia toharani, hiyo ni kusema, kuzitakasa nafsi zetu kwa Roho Wake Mtakatifu, kutokana na dhambi zetu, tukijaribu kuishi kitauwa kadiri tujuavyo kuishi katika wakati huu wa sasa, tukikutazamia kuonekana Kwake wakati wowote. Nasi tunalitazamia hilo wakati wowote.

5 Sasa, tuna ra—tatiba kubwa leo hii. Tuna ibada zetu za shule ya Jumapili hapa asubuhi ya leo, na halafu usiku wa leo tuna ra—ratiba maalum sana usiku wa leo. Rafiki yangu mwema, Ndugu Joseph Boze, ambaye, yeye si mgeni hapa pamoja nasi, bali ninaamini ndiyo mara ya kwanza amepata kututembelea kanisani. Ni . . . Daima nilikuwa na makanisa mawili ulimwengu mzima ninayotembelea, ambayo sikuzote ninayaita "makanisa mfano," na moja la hayo lilikuwa ni Ndugu Joseph Boze, lile Kanisa la Filadelfia huko Chicago, Illinois, na hilo lingine lilikuwa ni Ndugu Jack Moore, Shreveport, Louisiana. Nilikuwa kwenye makanisa hayo sana hata niliporudi nyumbani kutoka kwenye ziara ya kimishenari mtu fulani anasema, "Usipige simu Jeffersonville kumpata Ndugu Branham, ipige tu Chicago. Asipokuwako kule, vema, basi piga simu huko Shreveport." Nilikuwa huko sana.

6 Joseph amehama Chicago. Iliivunja mioyo yetu, mara ya kwanza, tulipowazia ilimbidi kuhama Chicago, bali baada ya maombi tukakuta ilikuwa ni Mungu akimpa wito. Basi maskini huyu rafiki yangu sasa ametangulia kuingia katika huduma kubwa ndani ya Tanganyika na Kenya na Uganda, naye anafanya kazi kubwa. Nasi tunajisikia kusaidia kumwunga mkono katika kila njia tuwezayo katika mikutano hii. Nami ninapanga, yakiwa ni mapenzi ya Mungu, mnamo Januari hii ijayo, kuwa pamoja naye kwenye shule zake kote katika Afrika kule, wakati tukiingia Afrika Kusini kutoka kwenye shule zake. Naye atawaambia zaidi juu yake usiku wa leo katika hotuba yake kwa kanisa. Atakuwa akizungumza alasiri ya le—leo kuhusu, nadhani yapata saa mbili, mara baada ya matangulizi kumalizika. Halafu anayo sinema mtakayofurahia kuiona, nina hakika. Nayo sinema hiyo ni ya shule zake katika Afrika, na yale Bwana amemfanyia katika muda mfupi tu miaka michache. Linanitia moyo sana kuonyesha jinsi . . . kuiona hiyo sinema, kwa sababu inaonyesha yale Mungu anayoweza kufanya na mtu mmoja atakayepata mapenzi na mahali Pake. Baada ya kungojea kwa miaka kadhaa kuyapata, kisha kutembea katika njia ambayo Mungu alimwongozea. Njoni pamoja na watoto, sehemu yake ya kwanza ni sehemu ndogo sana.

7 Kama mjuavyo, Joseph, wengi wenu, ana ucheshi mwingi. Nami nadhani alifikiri nitakuwa nikiitazama picha yake, kwa hiyo anatoka nje usiku mmoja na alitaka kupiga picha ya simba. Huko Afrika, kunao simba wengi. Kwa hiyo Joseph anatoka anaenda na kumpiga simba picha. Nami nilifikiri alikuwa ni kitu cha kupendeza mno. Akina mama wakiisha kuua, na wakiisha kumla mnya—mnyama huyo, alikuwa akiitoa ngozi. Ndipo maskini mtoto wake akimfuata nyuma, akijaribu kujifanya kana kwamba alikuwa akijaribu kumwua tena, mnaona. Basi nina hakika hao jamaa wadogo wataifurahia, nadhani, dakika tano ama kumi za hilo mwanzoni mwa sinema. Sasa, njoni mapema.

8 Na mimi sijaombwa kusema jambo hili. Sitaki kulisema. Joseph hajui lolote kulihusu. Bali nafikiri usiku wa leo tutaonyesha shukrani zetu kwa Ndugu Joseph kwa kumtolea sadaka ya misheni zake za nchi za ng'ambo. Tunaamini ya kwamba Bwana Yesu yuaja. Basi—basi kama umekuwa ukiweka akiba sadaka kidogo ya umishenari, ama kitu fulani kwa ajili ya wamishenari, ama kitu fulani ambacho ungetaka, mchango kwa hilo, andika tu hundi yako kwa Joseph B-o-z-e, usiku wa leo. B-o-z-e, hiyo ni kweli, sivyo? Joseph Boze. Na ni. . .ninamjua Ndugu Joseph kama rafiki yangu msiri, rafiki yangu binafsi, nami najua zitatumiwa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, kadiri ajuavyo yeye Kwake.

9 Na, hivyo basi, kabla hatujaendelea mbele zaidi, ningetaka kumtambulisha na kumwacha aseme neno moja hapa. Nilijaribu kumfanya aichukue hii ibada ya asubuhi, naye asingefanya hivyo, kwa hiyo yeye atatuzungumzia usiku wa leo saa mbili, kwa muda anaotaka. Nayo kamera itawekwa, na skrini hapa, kwa ajili ya sinema. Lakini sasa hivi ningetaka tu kuliambia kanisa, na kulijulisha kanisa rafiki yangu mwema na ndugu, Joseph Boze. Ndugu Boze.

[Ndugu Boze anazungumza kwa dakika tisa—Mh.]

Asante, Ndugu Joseph, hilo ni zuri sana. Bwana na abariki. Hii ni Uswidi na Ayalandi, pamoja. Mungu akubariki, Ndugu Joseph. Asante kwa pongezi zako, Ndugu Joseph. Ni, ninaweza kusema yayo hayo kumhusu yeye. Tunamshukuru sana Bwana kwa kazi yake kuu inayoendelea huko Afrika, naye atawaambia mengi zaidi juu yake usiku wa leo.

10 Na sasa naamini Billy alitokea polepole na kuniambia nimwambie Ndugu Neville ama mtu fulani. . .Sa—sauti si nzuri sana huko nyuma. Ama labda. . .Mwaweza kusikia huko nyuma vizuri? La, hawasikii vizuri sana. Waweza kuurekebisha mtambo?

11 Nami ninaamini, tunapomngojea afanye hivyo, ninaamini mpwa wangu, Donna, anaye maskini. . .yeye na Teddy wanaye jamaa mdogo hapa wanayetaka awekwe wakfu kwa Bwana. Na kwa hiyo, Donna, kama utamleta jamaa huyu mdogo sasa, mbona. . .Basi, hebu tuone, yuko wapi yule dada kwenye piano, yule mchezaji, yupo?

12 [Ndugu Edgar Branham anasema, "Tumia moja ya maikrofoni zilizo pembeni, mpenzi."—Mh.] Hii hapa? ["Hiyo ni sawa."] Vema, bwana. ["Yoyote ya hizo itafika."] Hiyo itakuwa sawa. Vema. Nilikuwa. . .Nilikuwa mahali pabaya. Nafikiri mimi ndiye niliyekuwa mahali pabaya.

13 Sasa, tunao wimbo mdogo ambao tumezoea kuimba yapata wakati huu kwa ajili ya hawa jamaa wadogo, huo ni, "Waingizeni, waleteni watoto wadogo kwa Yesu." Sasa katika. . .

14 Makanisa mengi huwanyunyizia jamaa hawa wadogo, na hilo ni sawa kama wanataka kufanya hivyo, hilo ni sawa kabisa kadiri ninavyohusika. Nao wengine wanazo njia ambazo wao, labda, ambazo wanaliita hilo ubatizo, basi kama wanataka kuliita hilo ubatizo hiyo ni sawa, kadiri ninavyohusika.

15 Ila Maandiko ndiyo tunayojaribu kufuata jinsi tu Biblia isemavyo, tunadumu tu katika Maandiko. Hakuna mahali katika Biblia, katika Agano Jipya, ila pale walipowaleta watoto wadogo kwa Yesu na Yeye akawabariki, na kusema, "Acheni watoto wadogo waje Kwangu, kwa kuwa walio kama hao Ufalme wa Mbinguni ni wao." Sasa, hivyo ndivyo tunavyolifanya. Mimi na mchungaji tunasimama pale, tunamchukua mtoto mchanga na kufanya maombi ya kuwekwa wakfu kwa Bwana. Ndipo wakati wanaponinii . . .

16 Tunajisikia kwamba mtoto mchanga hana dhambi, si zaidi ya kwamba alizaliwa katika dhambi. Sote tumezaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja ulimwenguni tukisema uongo. Na, sasa, Yesu alipokufa pale Kalvari, Yeye aliziondolea mbali dhambi za ulimwengu. Ndipo huyo mtoto angaliweza kuzaliwa, ama huenda angekufa kabla hajazaliwa; ama akazaliwa kabla hajafikia umri wa kuwajibika, yeye hana dhambi. Yesu aliziondolea mbali dhambi za ulimwengu. Lakini akiisha kuwa mkubwa vya kutosha naye atende dhambi, basi hana budi kuungama dhambi zake na kisha abatizwe kwa ondoleo la dhambi zake, mnaona. Lakini sasa, bila shaka, yeye ni mdogo mno.

17 Sasa, hebu sote tuuimbe wimbo huu mzuri wa kale sasa, tuimbe sasa. Sijui kama ninaweza kuongoza ama la.

Leta . . . ndani, waleteni,
Waleteni kutoka maeneo ya dhambini;
Waleteni, waleteni,
Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

18 Jina lake ni nani? Teddy, Junior. Vema, bwana. Tuna furaha sana kuwaona mume na mke hawa wachanga hapa asubuhi ya leo pamoja na mtoto huyu mzuri Teddy hapa, na tunaomba kwamba Mungu atambariki sana, na kumpa Uzima wa Milele katika ulimwengu ujao, na maisha marefu hapa. Naweza nimchukue kwa dakika moja? Huyu ni mtoto Teddy Arnold. Sote tunamjua Teddy hapa, yeye ni nanii wetu . . . ndugu hapa kanisani, amemwoa binti ya ndugu yangu hapa, Donna. Nao wanaye mtoto huyu mchanga hapa, mgeni. Nafikiri huyu ndiye wenu wa pili. Naye huyo mwingine ni msichana mdogo, hiyo si ni kweli? Yeye ni jamaa mdogo anayeonekana mwangavu. Sikuzote ninahofia nitawavunja wanapokuja wadogo hivi, te— teketeke sana, ninahofia tu watavunjika.

19 Sasa ungeweza kuwazia mama akimleta mtoto wake mdogo namna hii kwa Bwana Yesu? Kama angalikuwa hapa

asubuhi ya leo, mtu kama tunavyosimama, mama huyu upesi angemkimbilia, akimtaka aweke mikono Yake juu ya mtoto huyu mchanga na kumbariki. Moyo wa baba ungeruka kwa shangwe. Tunajua ya kwamba Mungu amewapa huyu kwa ndoa yao nao wanataka kumrudishia Mungu katika shukrani za Yeye kuwapa wao. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

20 Baba yetu wa Mbinguni, tunajaribu kufuata mfano Wako. Wakati akina mama na baba walipokuletea Wewe watoto wadogo, uliweka mkono Wako juu yao na kuwabariki. Na sasa, Baba wa Mbinguni, huyu mume na mke vijana wamebarikiwa katika nyumba yao, kwa kumpokea mvulana huyu mdogo, mtoto Teddy Arnold, Junior. Kwa hiyo tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba baraka Zako zikae juu ya huyu mtoto. Tunaweka mikono yetu juu yake katika kumbukumbu Yako na ahadi Yako kwetu, kwamba inatupasa kuweka mikono yetu juu ya watu katika kumbukumbu ya Neno Lako kuu. Mbariki mtoto Teddy. Mungu, tunaomba ya kwamba utampa maisha marefu, afya njema. Jalia aishi kukuona Kuja kwa Bwana, kama hiyo inawezekana. Nasi tunawaombea baba na mama yake, jalia wabarikiwe kwa kumlea mtoto huyu. Na kukiwako na kesho, mfanye mhudumu, Bwana, wa Injili, na umpe vitu ambavyo Wewe umeiahidi jamii ya binadamu, apate uzima, na Uzima kwa wingi. Tunakupa Wewe sasa, mtoto Teddy Arnold, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

21 Mungu awabariki, Donna na Teddy, maisha marefu na baraka nyingi; na kwako, mtoto Teddy, maana Yeye anakupenda.

22 Loo, nafikiri ni warembo sana, mimi...jamaa wadogo. Ninawapenda watu wote, bali nafikiri watoto na, halafu, wazee, unapozeeka. Mwanamume fulani mkongwe ama mwanamke wametoka mbali, na ni wanyonge sana, nami nafikiri wao ni wa kuhurumiwa tu, mwajua, nami nafikiri tu haitupasi... Ukiwaona wakivuka barabara, simama. Vipi kama huyo alikuwa ni baba yako ama mama yako? Unaona? Ni wa mtu fulani, kwa hiyo waheshimuni. Nao huzungumza labda polepole na kwa muda mrefu, na labda ni mambo usiyopenda kuyasikia, lakini, kumbuka, huenda wewe ukazeeka, pia, siku moja, kwa hiyo sikuzote waheshimu.

23 Nao hao jamaa wadogo, ni nani anayeweza kumwudhi mmoja wao? Jambo lingine, hupaswi kamwe kufanya hivyo. Mnajua, Yesu alisema, "Angalieni msidharau mmojawapo wa wadogo hawa, kwa kuwa malaika wao sikuzote huutazama uso wa Baba Yangu aliye Mbinguni." Kumbukeni, wanaye malaika. Unapozaliwa, yeye hukaa pamoja nawe kote maishani. Na sasa, ndipo unapookoka, unaye Roho Mtakatifu basi, naye Huyo hukuongoza na kukuelekeza.

24 Na sasa ninaangalia moja kwa moja kwenye kusanyiko kuona wale ninaowajua. Na, kama sijakosea, ninamwona dada kutoka Chicago hapa nje; hilo linakufanya kidogo ujisikie

nyumbani, kuwakilishwa katika Chicago, Dada Peckinpaugh na wote hao njiani mle. Tuna furaha asubuhi ya leo kumwona Ndugu na Dada Cox hapa; na Charlie, Nellie, tuwajuavyo. Na Rodney yuko hapa mahali fulani, nadhani, Dada Cox. Na Ndugu Willard Crase, mmoja wa ndugu zetu wahudumu hapa. Na wengi sana mbalimbali ambao nisingeweza kuwafikia nikawataje wote.

25 Nina furaha kumwona Ndugu Evans na Dada Evans huko nyuma. Huyo ndiye yule mtu niliyekuwa nikiwaambia aliumwa na nyoka mchacharisha, naye Bwana. . .Naomba uinue tu mkono wako ama kitu fulani, Ndugu Evans, kusudi waweze kuona mle ndani ya kwamba—kwamba ninii. . .Tulikuwa tukivua samaki, naye mchacharisha wa ardhini akamuuma papo hapo mguuni mwake. Kisha nikaweka mikono juu yake na kumwombea, na hata haukumwuma, ama kamwe hakuushughulikia hata kidogo baada ya hayo. Nayo Biblia ilisema, mwajua, "Watatoa pepo; watakanyaga vichwa vya nge na nyoka, wala hakuna kitakachowadhuru; na—na ninii yao. . . katika Jina Langu, hao waniaminio Mimi," vile nguvu zote na yale watakayofanya, na kadhalika, tulipewa. Ndipo, ikiwa tu wewe huogopi!

26 Vipi kama mtu alikupa hundi na ilikuwa na jina limetiwa sahihi hapo chini yake, na kama ukiibeba hundi hiyo mfukoni mwako maishani mwako mwote, ha—haitakufaa kitu. Huna budi kuigeuza kuwa pesa. Kwa hiyo, kila ahadi katika Biblia ina Jina la Yesu limetiwa sahihi hapo chini yake. Benki ya Mbinguni inawajibika, nayo amana iliwekwa Kalvari hapo dhambi zetu ziliposamehewa, sisi tumefanywa wana na binti za Mungu. Na hivyo basi usiogope kupokea karama yoyote ambayo Mungu aliahidi. Kumbuka tu, Yeye aliiahidi na ni yako.

27 Nimemwona Yeye akizima miali ya moto, akaikomesha damu, akakomesha shambulizi la—la ibilisi, na kuwatupa nje maadui, na kuponya kansa, kuwafufua wafu wakati daktari akisimama hapo, amekufa kwa saa kadha wa kadha, kafufuliwa moja kwa moja kuwa hai tena. Nimeyaona hayo katika maskini huduma yangu dhaifu, wakati baada ya wakati baada ya wakati. Nimewaona wanyama mwitu wametiishwa moja kwa moja hata wasingeweza kujongea, na mambo yote. Kwa hiyo Yeye ni ninii tu. . .Angali ni Mungu. Yeye. . .Kama aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Na kama Yeye—na kama Yeye kamwe. . . Na kama Yeye si Mungu, kamwe hajawahi kuwa Mungu, maana ingembidi kuwa. . .Ili awe Mungu, ingembidi kuwa asiye na kikomo, Yeye alijua mambo yote, ingembidi kuwa mwenye nguvu zote, mwenye uweza wote, ajuaye yote, aliyepo kila mahali. Na, loo, Yeye ni Mungu tu! Ukamilifu wa ukamilifu ni Mungu.

28 Sasa, simaanishi kuninii, wakati mwingine ninapofundisha madarasa haya ya shule ya Jumapili ni kama saa kumi, Joseph. Hapa Jumapili chache zilizopita, nilikuwa hapa saa sita. Sitaki

kuwashtua, mnaona. Lakini—lakini simaanishi hilo asubuhi ya leo; saa tano tu na nusu. La. Hii tu . . .

29 Huenda nisiwe pamoja nanyi kwa kitambo kidogo sasa, tunaelekea Virginia, ama mpaka huko Carolina, na Carolina ya Kaskazini na ya Kusini, kisha tuelekee Pwani ya Magharibi, na kukwea juu huko Pwani ya Magharibi, kisha tuingie Canada na Alaska, halafu turudi. Na labda, Bwana akipenda, tuende Afrika na kumwona Joseph, na kushuka kuingia Afrika Kusini tena.

30 Na tulikuwa na mkutano mkubwa sio muda mrefu uliopita huko Afrika Kusini, wakati ilipobadilisha mwelekeo wote wa Afrika katika saa chache tu, wakati Mungu, katika mambo Yake ya kimiujiza, ambapo kurasa za mbele za magazeti ziliandika makala hiyo, kurasa nzima ya kwanza na ya pili na ya tatu hakuna kitu ila makala tu juu ya hiyo mikutano. Mara ya kwanza kwenda kule, waliikataa tu kabisa, hata wasingempa mtu petroli kwa kuwa alikuwa akienda mkutanoni, wasingemwuzia, kasema, "Mtu yeyote mshupavu jinsi hiyo!" Ndipo kesho yake, walikuwa radhi kumpa petroli bure. Mnaona? Kwa hiyo ni hiyo tofauti tu, mnaona. Mimi . . . Jambo fulani linatukia. Alikuwa akibembeleza maskini chipukizi pale, mwajua, naye akamwambia, kasema, "Unaenda wapi?"

Akasema, "Ninashuka kwenda Johannesburg."

Kasema, "Loo, wewe ni mfanyabiashara?"

31 Kasema, "La, ninashuka kwenda kumwona Ndugu Branham, ule mkutano."

32 Kasema, "Ati nini?" Kasema, "Unaonekana u mtu mwenye akili kuliko hivyo."

33 Akasema, "Vema," kasema "Mimi ni Mkristo. Ninashuka kwenda kuuona."

Akasema, "Endesha uende mahali pengine ukajinunulie petroli."

34 Na kwa hiyo kesho yake, akirudi, kilikuwa ndicho kituo cha pekee kati ya pale na Transvaal, kwa hiyo ilimbidi kupitia pale, naye akasimama kwenye kituo kingine chini ya hicho. Ndipo jamaa huyo akakimbia na kumwita, kasema, "Njoo huku. Njoo huku juu." Magazeti yalikuwa na kurasa zote za mbele na kurasa za pili, na kadhalika, zilizojaa hayo, yale Bwana wetu aliyofanya. Na kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya hilo.

35 Sasa, kwa ajili tu ya kukusanyika pamoja kidogo, yeyote wenu ajaye, mmewahamasisha marafiki wenu, tutakuwa kwenye Ikulu ya Ng'ombe sasa. Ni mahali mashuhuri sana pa mifugo, maonyesho ya mifugo ya magharibi kwenye Pwani ya Magharibi, kwenye Lango la Kusini. Kwa hiyo baadhi yenu jamaa kama mimi, wanaopenda bunduki, nitapitia kwenye Kiwanda cha Weatherby kule, nanyi mwambatane nami mkipenda, iwapo mko karibu na pale. Na kwa hiyo wanaenda mahali pengi mchana

kutwa, mnaweza kwenda kwenye Kisiwa cha Catalina, mnajua jinsi kilivyo. Nanyi wanaume, wanawake pamoja na watoto wenu wadogo, Disneyland. Naye ni mmoja wa wanachama wa kundi hilo, pia, kwa hiyo njoni moja kwa moja. Ninyi, ninajua mtakuwa na wakati mzuri. Na, zaidi ya yote, ombeni kwamba Mungu atayafungua macho ya wasioamini na atawafanya waongofu kwa Kristo.

36 Sasa tutasoma Maneno machache tu kutoka kwenye Biblia hapa, kwa sababu ninapenda kufanya hili. Halafu ninayo Maandiko yalioandikwa hapa chini, humu ndani, na muhtasari ambao ningetaka kufundishia asubuhi ya leo, kwa dakika chache, nikikumbuka ibada ya usiku wa leo. Halafu ningetaka kuwaambia yote yaliyotukia juma hili katika mahojiano ya faraghani, na kadhalika, bali sina wakati. Nami nimeona wengine wao wameketi hapa asubuhi ya leo, ambao wangali wanayangojea mahojiano hayo, kutoka nje ya mji. Tutajaribu kuwafikia juma hili, upesi. . .kujaribu kupata kila kitu kinachongojea hapa, kwa vyovyote vile, kabla hatujaondoka.

37 Sasa tunataka kufungua katika Injili, kwenye Marko 16, mlango wa 16 wa Marko Mtakatifu. Nalo somo langu leo, la hili, ni *Uinjilisti Wa Wakati Wa Mwisho*. Basi hebu tuanze kusoma kwenye Marko 16, yapata kifungu cha 14.

> Na baadaye *akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa* mioyo yao, *kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.*
>
> *Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.*
>
> *Aaminiye na kubatizwa ataokoka;. . .asiyeamini, atahukumiwa.*
>
> *Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;*
>
> Nao *watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono* yao *juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*
>
> *Basi Bwana baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.*
>
> *Nao wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao,. . .kuthibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo. Amina.*

38 Kunayo mengi sana yangeweza kusemwa juu ya hili. Hili ndilo agizo la mwisho la Bwana alilolipa Kanisa.

39 Mimi ni. . .imetokea nimeangalia chini hapa. Ninajaribu kuwazia. . .Ndugu West, nilikuwa nikijaribu kulikumbuka jina lako dakika chache zilizopita, unayeketi hapo kutoka Georgia.

Nami kamwe nisingeweza kukumbuka jina lako lilikuwa nani, dakika chache tu zilizopita. Huyo ndugu mwingine anayeketi hapo, siwezi kulikumbuka jina lake. Na wengi sana wa... Mnaelewa sijaribu kujifanya simjui mtu fulani, bali wao wananinii tu... Siyaweki majina yao sana akilini mwangu.

40 Sasa tunawazia juu ya uinjilisti kwenye wakati wa mwisho. Na mtu yeyote ambaye angeninii, angeweza kusoma gazeti, na angeweza kusoma... Anga ni nyeusi na zinaingia giza, nayo wawingu yanatanda, na—na anajua tuko karibu kupata mvua, anaweza kuihisi hewani, na kuona ile michirizi mikuu kwa mbali sana, na radi na kusukumiza kwa upepo, anajua tutakuwa na dhoruba, mvua itanyesha karibuni sana. Mtu yeyote anaweza kusoma gazeti na kuona hali ya taifa, mataifa, kutambua kwamba jambo fulani linakaribia kutukia. Mnapomwona mtu akiwa mkali kwa sababu ya kujiona amedharauliwa, na huyo mwingine, nao wanabishana, wakiwa na kila namna ya silaha na kadhalika za kupigana, wala hapana mapatano, wakivua viatu vyao na kupiga madawati na kila kitu kwenye makongamano yao, mnajua jambo fulani linakaribia kutukia. Na hilo linaleta juu ya watu namna fulani ya hisi ya kwamba jambo fulani liko karibu kutukia. Ulimwengu, kama vile tungeuita, kosmosi, ulimwengu wa nje, unahisi ya kwamba kunakuja maangamizi, ya tuseme kitu kama wakati wa atomiki unajiandaa kulipuka.

41 Mkristo anajua ni Kuja kwa Bwana. Mnaona? Kuna mazingira. Inategemea kile unachoangalia, kwa kuwa Bwana wetu ametwambia kinaganaga kile tu kilichokuwa kinaenda kutukia kwenye wakati huo, nasi hatujui hiyo dakika wala saa, bali tunajua kwamba tunakaribia kitu fulani sasa.

42 Kama nilivyokuwa nikizungumza hapa wakati fulani uliopita, nikimwangalia mwana-kondoo siku moja huko Afrika, kutoka kwenye boma, naye alikuwa—alikuwa akila nyasi kwa amani sana, ndipo mara ghafla akashikwa na wasiwasi. Basi nikashangaa imekuwaje kwa huyo jamaa mdogo. Nanyi mnajua kondoo hawezi kupata njia ya kurudi popote alipotoka, yeye amepotea kabisa. Hiyo ndiyo sababu Bwana hutulinganisha na kondoo, mnaona, tunapopotea, kuna kitu kimoja tu kinachoweza kuturudisha, yule Mchungaji. Basi maskini jamaa huyu alikuwa akilia, naye alikuwa ametangatanga kutoka kwenye boma. Ndipo nikaona, kwenye nyasi, huko chini kabisa, maskini jamaa huyo asingeweza kumwona. Naye mwana-kondoo ama kondoo hamnusi adui wake kama hao wengine, kama vile kulungu ama kitu kama hicho, lakini a—angeweza kuhisi kwamba mauti yalikuwa yamekaribia. Basi kulikuwako na simba aliyekuwa akinyemelea, akija polepole. Angeweza kumnusa huyo kondoo, kwa hiyo alikuwa akija, mnaona, kumshika huyo mwana-kondoo. Basi maskini jamaa huyo akashikwa na wasiwasi, nawe usingeweza kuona sababu yake, bali yalikuwa ni mauti yakivizia karibu sana hata akashikwa na wasiwasi.

43 Nao u—ulimwengu umeshikwa na fadhaa sana sasa hivi hata watakwenda barabarani wakiendesha maili tisini kwa saa, wakaketi kwenye baa na kunywa kwa muda wa saa mbili kabla hawajaenda nyumbani. Na ni mvamio wa . . .

44 Ukizungumza na mtu fulani, loo, jamani, wanalipuka! Kama nilivyokuwa nikizungumza hivi majuzi kwenye maskani fulani, na kuhusu kwenda hospitalini huku nje kujaribu kuichukua baadhi ya miito ya Ndugu Neville. Na kila wakati ningezungumza na nesi ama daktari, wangekukaripia, "Sijui lolote kulihusu!"

45 Vema, nikawazia, "Kwani kuna nini? Kila mtu anatoa tu presha, nadhani." Lakini, daktari, madaktari wa akili wanawatibu madaktari wa akili.

46 Kwa hiyo, bali kuna njia ya kuepukia, hiyo ni Kristo. Sasa, Mkristo hapaswi kuwa katika hali hiyo. Tunapaswa kuwa na furaha, tukikungojea kule Kuja, kwa kuwa kumekaribia. Tunaweza kuhisi upepo mwanana wa kubaridisha wa Kalvari. Tunapoangalia chini na kuona Mungu wa Mbinguni Yule aliyetoa ile ahadi, na mambo yale yale Yesu aliyofanya maishani Mwake, aliyoahidi yangerudi katika siku za mwisho, na hapa tunayaona. Ni kitu gani hicho? Hicho ni pumzi la kuburudisha, kama mvua ikija. Mnaona? Tunajua ukombozi umekaribia. Mnaona? Jambo fulani linakaribia kutukia. Sasa, ulimwengu hauoni hilo. Wanalicheka, kwa sababu kama walivyofanya katika siku zingine. Lakini tunajua linakaribia.

47 Na hiyo ndiyo sababu nilichagua leo hii somo hili, kuwa langu la mwisho kwa ajili ya maskani kwa kitambo kidogo, juu ya uinjilisiti wa wakati wa mwisho. Na wakati tunapofanya kazi ya kimishenari ama umishenari wa nchi za kigeni, pamoja na Neno la Mungu, tunajua daima tuko katika mapenzi ya Mungu, kwa sababu agizo la kwanza la Yesu kwa kanisa Lake lilikuwa ni "Enendeni mkaihubiri Injili." Agizo hili la mwisho lilikuwa ni kuihubiri Injili.

48 Mara ya kwanza Yeye aliyopata kuwaagiza watu wowote kulihubiri Neno na kwenda nchini kote, Yeye alisema, "Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure." Mathayo Mtakatifu, mlango wa 10, kuwatuma wale sabini, wawili wawili. Hilo lilikuwa ndilo agizo la kwanza alilolipa Kanisa Lake.

49 Sasa, agizo la mwisho alilolipa Kanisa Lake kabla tu hajapokelewa juu Utukufuni, alisema, "Enendeni ulimwenguni kote." Alikuwa tu amefufuka kutoka kwa wafu. Na wengi wao walikuwa wameketi pamoja, ndipo Yeye akawakemea kwa ajili ya ugumu wa moyo wao, kwa sababu ya kutokuamini kwao, ambao hawakuwaamini wale waliokuwa wamemwona akiisha kufufuka. Mnaona, walikuwa na ushuhuda kwamba walikuwa wamemwona Bwana. Basi wengine hawakuamini, ndipo

akawakemea kwa ugumu wa moyo wao. Hawakuwaamini watu hawa waliokuwa wameona kwamba Yeye hakuwa amekufa, "Yu hai!"

50 Jambo lile lile siku hizi, unapoiona kazi Yake. Sasa, tayari tumeona na kushuhudia kule kuonekana kwa Bwana. Sasa kumbukeni, kuonekana na kuja ni maneno mawili tofauti, kuonekana na kisha kuja. Sasa ni kuonekana, Yeye tayari ameonekana katika siku hizi za mwisho. Papa hapa pamoja nasi katika miaka michache iliyopita. Sasa, ni ishara ya Kuja Kwake. Yeye anaonekana katika Kanisa Lake, katika umbo la Roho Mtakatifu, akionyesha ya kwamba ni Yeye, maana watu hawawezi kuyafanya mambo haya mnayomwona Roho Mtakatifu akiyafanya, kwa hiyo huko ndiko kuonekana kwa Bwana. Sasa kumbukeni, imenenwa mahali pote pawili, "kuonekana" na "kuja."

51 Sasa, Yeye aliwakemea kwa sababu ya ugumu wa moyo wao, kwa sababu hawakuwaamini wale waliokuwa wamemwona. Ninaamini angefanya jambo lile lile leo hii. Baada ya sisi… Wameninii…hawakuamini ushuhuda wa watu wale, na Yeye akawakemea kwa ajili yake. Kisha akawaagiza waende kote ulimwenguni, wakaihubiri Injili kwa kila kiumbe, na Yeye angekuwa pamoja nao hata ukamilifu wa dahari, mwisho wa ulimwengu. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

52 Sasa, leo hii, tunajaribu kulichukua Neno lililoandikwa tulilo nalo katika umbo la herufi, umbo la kanuni za imani na kadhalika, ulimwenguni kote. Na kumekuwako na wamishenari walioenda kila mahali. Lakini tunapata nini tunapofika kule? Mwenyeji asiyeweza kulisoma jina lake, ameshika kitini mkononi mwake. Yeye hajui zaidi kukihusu kuliko anavyojua ni upi mkono wa kulia na wa kushoto. Lakini hapo Yesu aliposema, "Enendeni mkaihubiri Injili," Yeye kamwe hakusema "mkalifundishe Neno." Yeye alisema, "Mkaihubiri Injili!" "Nayo Injili haikuja kwa Neno pekee, bali kwa dhihirisho la Neno," kwa kuwa njia pekee hilo lingaliweza kufanywa ilikuwa ni kuifanya ahadi Yake itimie.

53 Jamaa fulani anaweza kulisoma hilo kama William Jennings Bryan, alipokuwa akijadiliana na Darreow juu ya maadili ya Darwin. Mnaona? Yeye angeweza tu kusema yale Darwin alikuwa amesema. Naye William Jennings Bryan angeweza kusema yale Biblia ilikuwa imesema. Huo ulikuwa ndio mjadala. Lakini, katika kisa hiki, Mungu anashuka miongoni mwa watu na kuthibitisha kwamba Neno Lake limedhihirishwa. Na njia pekee unayoweza kufanya hilo, sio kwa kitini, bali ni kwa Roho Mtakatifu akitenda kazi kupitia kwako. Uhai wako unakuwa uhai Wake. Yeye yuko ndani yako.

54 Wale makafiri, walipoiabudu sanamu yao, walisujudu mbele ya hiyo sanamu, na kuamini ya kwamba hiyo sanamu ilizungumza nao, mungu huyo, mungu wao aligeuka, akaingia

ndani ya sanamu hii na kuzungumza nao kuzipitia. Sasa, hiyo ni kinyume tu, walibadilisha kile Mungu alicho. Mungu hashughuliki na sanamu. Wewe ndiwe chombo Chake. Unasujudu mbele za Mungu, ndipo Yeye anaingia ndani yako na kuzungumza na watu. Hiyo ndiyo tofauti. Yeye ni Mungu aliye hai kwa ajili ya mtu aliye hai, sio Mungu aliyekufa kwa sanamu iliyokufa. Yeye ni Mungu aliye hai kwa mtu aliye hai. Nawe unakuwa shahidi Wake, yale Yeye aliyosema hapa.

55 Hiyo ni sasa, angalia, watu wengi wanasema kwamba hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya mitume pekee. Yeye alisema hapa, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili hii kwa kila kiumbe, na" (kiunganishi) "ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

56 Sasa, siku hizi, tunasema mfuasi mzuri wa kanisa hupeana mikono na mchungaji, anahamisha jina lake kutoka kwa Methodisti akaliingiza kwa Baptisti, ama Baptisti hata kwa Methodisti, ama kadhalika, na anaishi maisha mazuri sana. Sasa, sisi wamishenari, tunawaona hao makafiri wakiishi maisha ambayo Wamarekani hawa, wanaojiita Wakristo, wasingeweza kujilinganisha nayo kwa vyovyote vile. Mnaona? Kwa hiyo kama maisha mazuri ndiyo tu yanayojalisha, hao wameokoka sawa na hao wengine, kwa sanamu. Uadilifu wao ungetusonga hata tusingepata nafasi ya kusimama mbele zao, hiyo ni kweli, na matendo yao. Lakini hilo silo.

57 Yesu alisema, "Hamna budi kuzaliwa mara ya pili." Kusudi uzaliwe mara ya pili, ni kujiachilia uende na ufe, ndipo Roho wa Kristo anaingia ndani yako. Ndipo wewe si wa nafsi yako tena; ni Kristo ndani yako, unaona, Roho Mtakatifu. Paulo alisema, "Nakufa kila siku; hata hivyo ninaishi, si mimi, bali Kristo anaishi ndani yangu." Mnaona, Kristo!

58 Na kama niliwaambia roho ya John Dillinger ilikuwa ndani yangu, ningekuwa na bunduki hapa na niwe haramia, kwa kuwa hiyo ingekuwa ni roho ya—yake ndani yangu. Kama niliwaambia roho ya mwanasanaa, mngenitarajia kuchora picha ya mwanasanaa.

59 Kama nikiwaambia mimi ni Mkristo, na Roho wa Kristo yuko ndani yangu, ama ndani yako, basi tutafanya kazi za Kristo. Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu, "Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya." Ndipo akasema hapa, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

60 Sasa, kote katika wakati, kumekuwako na wakati ambapo ishara hizi hazijafuatana na waaminio. Hiyo ni kweli. Nabii alinena habari zake, naye alinena juu yake katika Zekaria, alisema, "Utakuja wakati ambao usingeweza kuitwa mchana wala usiku, lakini wakati wa jioni kutakuwa nuru."

61 Sasa, jua huchomoza mashariki na kutua magharibi. Halibadiliki, ni jua lile lile. Sasa wakati Roho Mtakatifu

alipokuja, Yesu, Mwana wa Mungu, Yeye alikuja mashariki, juu ya watu wa mashariki. Imekuwa ni siku. . . kama alivyosafiri, kama vile ustaarabu umesafiri pamoja na jua, ukitoka mashariki kwenda magharibi, na sasa tuko kwenye Pwani ya Magharibi. Tukienda mbele zaidi, tumerudi mashariki. Kwa hiyo, vema, kila kitu kinaonyesha Kuja Kwake. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Kila kitu kinaonyesha kwamba yote yamekwisha.

62 Sasa, sasa nabii alisema (Wala hakuna unabii unaoweza, unaopaswa kufasiriwa apendavyo mtu, kama Yesu alivyosema; ni vile tu hasa Huo unavyosema.): “Itakuwa nuru wakati wa jioni.” Basi Mwana yule yule aliyewajia watu wa mashariki na kuwaonyesha kazi Zake na baraka Zake, ilitabiriwa kwamba kungekuwako na siku ya utusitusi; si mchana wala usiku, hiyo ni siku yenye mawingu, hiyo kama ukungu. Na huwezi kuliona jua, bali hata hivyo jua linatoa mwangaza wa kutosha. Kitu kama ilivyo huko nje sasa, labda giza zaidi kidogo. Nasi tumekuwa na ya kutosha kujiunga na kanisa na kuandika jina letu kwenye vitabu, na kadhalika, bali wakati wa jioni nguvu zizo hizo kuu za Kristo zingekuja juu ya Kanisa Lake kama tu zilivyofanya huko nyuma mashariki. Magharibi itakuwa ni vile vile. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu ninataka kuzungumza juu ya uinjilisti wa wakati wa jioni.

63 Kila wakati umekuwa na ujumbe wake na wajumbe wake. Kote katika nyakati, kila wakati umeubeba ujumbe wake na mjumbe. Mungu, katika kila kipindi cha wakati, amemtuma mtu fulani aliyetiwa mafuta na Roho Mtakatifu, kuuleta Ujumbe Wake kwa ajili ya wakati huo, kila wakati.

64 Sasa, tungeweza kuanzia nyuma, kuliunga mkono kidogo tu. Hata tangu mwanzo, Mungu alikuwa ndiye Mjumbe hapo mwanzo, kuwaambia Adamu na Hawa, “Mtakula *hili*, bali hamtafanya *hili*.” Huo ulikuwa ndio Ujumbe. Ndipo mwanadamu alipouvuka Ujumbe wa wakati, ilisababisha mauti na machafuko kwa jamii yote ya binadamu. Sasa, hivyo ndivyo Ujumbe unavyomaanisha. Pia kumbukeni kwamba haikuwa ni kukanusha kinaganaga yale Mungu aliyosema, ambayo Hawa aliamini, ilikuwa ni kuchukua yale Mungu aliyosema na kuyapaka chokaa, ama—ama kuyafasiri vibaya kidogo tu, kuongeza kidogo tu Kwake, ama kuondoa kidogo kutoka Kwake.

65 Hiyo ndiyo sababu ninaamini ya kwamba Neno ni Kweli. Ikiwa kanuni zetu za imani na madhehebu yetu hayaambatani kabisa na Neno, basi yamekosea. Na ikiwa Mungu hataruhusu, nalo Neno Lake lilikuwa ni muhimu sana, kunukuu tu vibaya neno moja Lake kulisababisha yote, kila kifo kilichopata kutokea, kila mateso, kila mtoto mchanga anayelia, kila msafara wa mazishi, kila kaburi ubavuni mwa kilima, kila gari la kuchukulia wagonjwa lililowahi kupiga makelele, kila damu iliyowahi kumwagwa, uzee wote na kufa kwa njaa na matatizo ambayo tumekuwa nayo, kwa sababu tu Neno la Mungu

lilikosewa, kulisababisha haya yote, hivi Yeye atalisamehe wakati wa mwisho iwapo tutalikosea Hilo tena?

66 Kwa hiyo, mnaona, Ukristo ni kitu muhimu. Kama imegharimu miaka hii yote elfu sita ya shida, kwa sababu ya Neno moja kutumiwa vibaya, sasa hatutarudi na Neno lingine moja likitumiwa vibaya. Halina budi kuendana na Neno kabisa, pasipo na fasiri ya mtu yeyote, kile tu Neno lisemacho! Watu wengi sana watakutanika na kusema linamaanisha *hivi*, nao watakubaliana, na wengine watasema *hivi*. Lakini Hilo linasema, "Hili Ndilo!"

67 Kama Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa, basi ni kanisa lipi? Kama atalihukumu kwa taifa, ni taifa lipi? Yeye atauhukumu ulimwengu kwa Neno, Biblia. Kwa kuwa, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Huyo alikuwa ni Kristo, alikuwa ni Neno la Mungu lililofanyika mwili, lililonenwa kupitia kwa mwanadamu.

68 Sasa, katika Kitabu cha Ufunuo, Yeye alisema, "Kama mtu yeyote akiondoa Neno moja kutoka hapa, au kuongeza neno moja Kwake, huyo ataondolewa, sehemu yake, kutoka kwenye Kitabu cha Uzima."

69 Kwa hiyo mnaona sio tu, "Vema, ninaamini *hili*, bali sijui kuhusu *lile*." Inakubidi kuliamini lote. Labda huna imani ya kulistahimili Hilo, bali usijaribu kumzuia mtu mwingine.

70 Mara nyingi nimesema laiti ningalikuwa na imani, maisha yangu yakimalizika, kwenda kama Henoko, pasipo kufa, lakini nifanye tu matembezi ya alasiri na kwenda nyumbani pamoja na Mungu. Ningetaka kufanya hivyo. Lakini ikiwa sina imani ya namna hiyo, sitamzuia mtu mwingine aliye na imani ya namna hiyo. Mnaona?

71 Sasa, tuko katika wakati wa jioni. Nao wajumbe kote katika wakati. . .Tunaona ya kwamba hapo mwanzo wakati mjumbe alipotumwa, ku—kufasiri vibaya Neno Lake ama kutilia shaka Neno moja, ilikuwa ni maangamizi makamilifu na utengano wa Milele kutoka kwa Mungu, kufasiri vibaya Neno la mjumbe huyo. Naye Mjumbe wa kwanza alikuwa ni Mungu Mwenyewe. Na ninii. . .Kila mjumbe mwingine amekuwa ni Mungu akizungumza kupitia mwanadamu, tangu, ambalo ni Neno la Mungu, kwa kuwa hakuna mtu basi Kwake kuzungumza kupitia ila tu yule Yeye alikuwa akizungumza naye. Lakini tangu alipomwumba mwanadamu na kumkomboa mwanadamu, imekuwa ni Mungu akizungumza kupitia mwanadamu. Yeye hatumii wa—wakala wa—wa chombo chochote cha kimitambo, bali njia ya mwanadamu, mtu ambaye amajitolea na kujiweka wakfu kwa Mungu.

72 Jinsi ambavyo tungelishusha kupitia kwa manabii, na Samsoni, na kuendelea moja kwa moja hadi wakati uu huu wa sasa. Imekuwa daima ni mtu binafsi na Mungu. Sasa, kila wakati, nilisema, ulikuwa na ujumbe wake na mjumbe wake. Sasa tuchukue wakati mwingine baada ya wakati wa Edeni, kupata tu msingi kidogo. Sasa, baada ya wakati wa Edeni unakuja wakati wa Nuhu. Sasa wakati ulimwengu… tulikuwa…Nilikuwa nikizungumza hivi majuzi usiku huko kwenye maskani ya Clarksville, juu ya somo la ishara ya wakati wa mwisho. Na halafu hivi majuzi usiku, Alhamisi usiku, juu ya kutambulishwa na Yesu. Na sasa asubuhi ya leo juu ya mwinjilisti wa wakati wa mwisho, uinjilisti, samahani.

73 Sasa, kabla tu ya yale maangamizi yaliyoitangulia ile gharika na wakati wa ile gharika, vema, tunaona ya kwamba walikuwa na ustaarabu mkuu kuliko tulio nao siku hizi. Ninaamini walikuwa na udhibiti wa nguvu za atomiki. Nafikiri hizo ndizo zilizoutikisa ulimwengu kutoka kwenye mzingo wake. Nimesimama kwenye Maeneo ya Barafu ya Uingereza; wanachimba futi mia tano kwenda chini, wanatoa mitende, ambako kulikuwa na mitende kule, na mamia mengi ya miaka iliyopita. Nasi tunafundishwa na kujua kwamba ulimwengu ulisimama wima. Lakini, nao walikuwa na mitambo mikubwa sana na sayansi hata wangeweza kujenga piramidi, sfinksi, na kadhalika, ambazo tusingeweza kujenga tena siku hizi. Hatuna mitambo ya kunyanyua mawe hayo juu hivyo, mnaona, isipokuwa iwe ni atomiki; nguvu za petroli hazitamudu hilo, wala nguvu za umeme haziwezi. Lakini ulikuwa ni wakati mwingine mwerevu zaidi kuliko wakati wetu.

74 Basi katika wakati huo, Mungu alimwita mtu aitwaye Nuhu, mtu wa kawaida tu, mkulima, kwa kuwa alionekana kuwa mtauwa katika kizazi chake. Naye Mungu akashughulika na mtu huyo mmoja juu ya hoja ya "kujenga safina," kwa sababu, dhambi, tunaona kwamba katika wakati huo kwamba "Binti za—za wanadamu," Biblia ilisema, "waliwaona…wana wa Mungu waliwaona binti za wanadamu."

75 Kulijadili hilo, ambapo wengi wa waandishi huwazia kwamba hao walikuwa ni wana wa Mungu ambao malaika walioanguka walijisukumiza wenyewe katika roho. Sioni jinsi mtu angeweza kuwazia hilo. Hilo lingemfanya muumbaji, lingemfanya Shetani kuwa muumbaji. Shetani si muumbaji, Shetani ni mpotoshaji wa uumbaji, mnaona, wote. Uongo ni ukweli tu ulioelezewa vibaya. Uzinzi ni tendo la haki lililopotoshwa. Mnaona? Na hivyo ndivyo dhambi ilivyo hasa. Shetani hawezi kuumba, anaweza tu kupotosha kilichoumbwa.

76 Kwa hiyo ilikuwa ni wana wa Mungu, ambao walikuwa ni wana wa Sethi kutoka kwenye ukoo wa Mungu, kupitia Adamu; nao binti za Kaini, Shetani, "Ndipo walipowaona ya kuwa ni warembo, wazuri."

77 Nasi tunaona mle ndani, ya kwamba tukileta picha ya kama miaka michache iliyopita, tuseme miaka mia moja iliyopita, jinsi ambavyo urembo wa wanawake umepita urembo uliokuwamo katika wanawake. Iwapo utasoma Mwanzo 6, utaona picha yake nzuri pale. Walikuwa ni warembo. Nao wanawake siku hizi ni warembo zaidi ya walivyokuwa. Ni kwa sababu ya nguo zao na mtindo wao mamboleo. Hizo ndizo zinazowatoa.

78 Ninayo picha ya Pearl White, alivyokuwa wakati Scott Jackson alipomwua, akamchoma kisu kifuani mwake, yule mpenzi wa kisiri, ndipo hili taifa kuu likatikisika kwa ule wimbo wa Pearl White. Alidhaniwa kuwa mwanamke aliye mrembo kuliko wote aliyekuwako ulimwenguni katika siku hizo. Mbona, angekuwa ni mabaki ya binadamu mtaani siku hizi, kwa baadhi ya wanawake hawa.

79 Ama, rudini kwenye wakati wa Clara Bow, wakati alipoanzisha ile kashfa ya kukunja soksi zake ndefu chini ya magoti yake, na kusema, "Zikunjeni 'izo, enyi wasichana, zikunjeni 'izo." Ninakumbuka hayo katika ujana wangu. Basi chukua ile picha ya Clara Bow ukailinganishe na baadhi ya hawa warembo wa siku hizi. Unaona?

80 Na hiyo ni ishara ya wakati wa mwisho. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu." Nao wanaendelea kujivua nguo. Ni kitu gani hicho? Binti za Kaini. Hiyo ndiyo sababu tunahesabiwa kuwa wenye kichaa na washupavu tunapojaribu kuelezea na kuutangaza ukweli wa Injili kulihusu. Lakini wanaendelea kujipotosha na kuingia mitaani na—na kutenda jinsi wanavyotenda, wala hawatambui kwamba watawajibika kwenye Siku ya Hukumu. Sasa, mwanamke ambaye hujivalisha vibaya, kizinifu, na labda huenda ukawa safi kama yungiyungi kwa mumeo, ama kwa mpenzi wako, mpenzi wako wa kiume, bali hapo huyo mwenye dhambi anapopitia mtaani na kukuangalia nawe umevalia jinsi hiyo, atakutamani kwa kuwa umejianika kwake jinsi hiyo.

81 Sio watoto wanaohitaji kucharazwa, ni baba na mama, kwa kuwaacha wafanye hivyo. Hiyo, si upotovu wa watoto, ni upotovu wa wazazi. Nami nadhani ni upotovu mwingi wa mimbarani, kwa kuwa wanawaachilia tu pasipo kusema kitu juu yake, wakati likiwa hapo kwenye Neno.

82 Sasa, sasa Biblia, Yesu alisema, "Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha," wakati uliopita, "kuzini naye moyoni mwake, tayari." Basi wakati mwenye dhambi huyo anapoenda hukumuni apate kuwajibika kwa ajili ya uzinzi, itaruka nyuma mara moja, "Kwani ulitenda dhambi na nani?" Na wewe! Ingawa kamwe hukutenda tendo hilo, bali Biblia ilisema una hatia, kwa vyovyote vile. Ni nani wa kulaumiwa basi? "Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa

kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Ule uzito wake!

83 Huko Jeffersonville siku hizi, kuna asilimia tisini na tisa na tisini na tisa juu ya kumi ya wanawake walio na hatia mbele za Mungu. Taifa zima liko hivyo. Kwa nini? Upotovu mimbarani, kuwaambia watu; na upotovu nyumbani, kuwaachilia wasichana waende mtaani na kutenda jinsi hiyo. Nao wanaliita "vema."

84 Sasa, hilo hasa ndilo lililombidi Nuhu kushindana nalo katika siku zake. Binti za wanadamu walikuwa ni warembo, nao wana wa Mungu wakawatazama. Mnaona, ile tamaa ikirudi tena. Bali Nuhu, loo, tungekaa hapo saa kadhaa. Lakini Nuhu alikuwa mtu wa haki, mtauwa, mwadilifu, naye aliyakemea hayo. Nao wakamwita mwendawazimu. Wenye kudhihaki, Biblia ilisema, kwamba walimdhihaki, wakamfanyia mzaha. Ila yeye alisema, "Unakuja wakati ambapo dhoruba, maji yatatiririka kutoka angani." Kamwe hakukuwa kumewahi kuwa na mvua. Wala Injili yake haikustahimili nadharia zao za kisayansi za siku hiyo, kwa kuwa hapakuwapo na mvua angani.

85 Na, siku hizi, nadharia ya kisayansi ya wanaojiita makundi mamboleo ya kidini imejaribu kuthibitisha kwamba Kitu hiki kilichobarikiwa tulicho nacho, kinachoitwa Roho Mtakatifu, ni muhemko tu. Mnaona, kamwe hakiendani na nadharia yao ya kisayansi. Vema, ningetaka kuwauliza jambo hili, ni kitu gani kinachowafanya wabadilike? Ni kitu gani kinachomfanya mlevi kuacha kunywa pombe? Ni kitu gani kinachomfanya kahaba kuyaacha maisha yake maovu? Ni kitu gani kinachofanya kansa na—na magonjwa yawaache watu, na viziwi, bubu, na vipofu, na wafu kufufuka? Elezeni jambo hilo. Kwani huo ni muhemko? Linaambatana na muhemko, bila shaka.

86 Chochote kilicho hai kina muhemko, na chochote kisicho na muhemko kimekufa. Samahani hili tamshi, bali ninawazia tunapaswa kuzika baadhi ya dini zetu zisizo na muhemko, maana zimekufa. Haina muhemko kwake. Dini yoyote isiyo na muhemko inapaswa kuzikwa, a-ha, kwa sababu, Hilo lina muhemko!

87 Yesu, alipoingia mjini, watoto na hao wote, marafiki Zake wote, walishangilia, "Hosana! Yeye ajaye katika Jina la Bwana!" Ndipo hao wenye dini wa siku hizo wasingeweza kuvumilia hilo, ilikuwa na muhemko mwingi mno. Yeye akasema, "Wakinyamaza, mawe yatapiga kelele mara moja." Mnaona? Kitu fulani hakina budi kupiga kelele, kwa kuwa uhai ulikuwemo.

Nuhu alikuwa na wakati mgumu sana, bali hatimaye siku moja alikuwa na jaribio.

88 Nao wote wanaoambatana na Mungu wana majaribio, imani yako inajaribiwa. Unapoanza kumwishia, basi kila jirani atanena habari zako, kila kitu kitaenda mrama kwako.

Kumbuka tu hilo, kwa kuwa ni Mungu akikujaribu. Biblia ilisema, "Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kuthibitishwa kwanza, kurudiwa, kufunzwa kama mtoto." Kama vile baba yangu alivyonifundisha nilipofanya kosa, walikuwa na—walikuwa na zile—zile amri kumi zimetundikwa juu ya mlango, ulikuwa ni mjeledi mrefu karibu *hivi*; naye Bw. Branham alikuwa hodari sana mkononi mwake, naye alitupeleka nje akatufunza. Na hivyo ndivyo Mungu afanyavyo. Yeye hukujaribu, anakufunza kama mtoto, anakulea, kwa sababu wewe ni mtoto Wake; kuna kitu fulani katika siku za usoni kwa ajili yako, makazi Utukufuni. Naye hukufunza. Sasa, kila mwana ajaye hana budi kujaribiwa.

89 Nuhu, mfano sasa wa majira yake ya wakati, alikuwa na jaribio, maana Mungu alimwambia aingie safinani, ndipo alipoingia katika safina, mlango ulijifunga wenyewe. Naye Nuhu hapana shaka aliiambia familia yake, "Tazameni kesho. Loo, mlango ulijifunga usiku wa leo, bali asubuhi kutakuwako na mvua huko juu angani." Kamwe haikuweko hapo kabla, kumbukeni.

90 Nao wenye kudhihaki, labda baadhi yao kidogo ni waaminio nusu, walisema, "Hebu tupande tukasimame. Mwajua, maskini mzee huyo huenda alisema kweli." Wakasimama kuizunguka ile safina, wakingojea, mwajua, na kuwazia, "Vema, sasa, huenda alisema kweli." Basi wakakwea. Ndipo kesho yake asubuhi, jua lilichomoza vizuri vile vile, likatokea.

91 Mwajua, na hapana shaka ila kwamba Shetani aliketi kule juu ya shimo hilo safinani, lile dirisha, kasema, "Unafikiri ungali sahihi?" Vema, hivyo ndivyo ibilisi anavyotufanyia sote. Lakini maadam Mungu alisema hivyo, dumu na Hilo! Hilo halijalishi hata, dumu moja kwa moja na Hilo.

92 Siku ya pili ikapita, siku ya tatu ikapita. Nuhu aliwaza na kuwazua. Lakini, hatimaye, baada ya siku saba! Na hiyo ilikuwa ni tarehe 17 Februari wakati alipoingia ndani. Ndipo baada ya siku saba, basi asubuhi hiyo hapo alipoamka, ngurumo zilikuwa zikinguruma, matone makubwa mno ya mvua yalikuwa yakianguka kote. Wale waliokuwa wamekwea na kukaa siku moja ama mbili, wapate kujua, wakasema, "Vema, tutaenda tuone kama lolote litatukia," muda ulikuwa umeenda sana wakati huo. Walibisha, wakapiga mayowe. Mitaa ikafurika maji, yakaanza kupanda ubavuni mwa vilima. Watu wakakimbilia milimani. Wakajaribu kuwaweka kwenye mitumbwi, na kadhalika, bali ikiwa huo mtumbwi haukuwa umeundwa na Mungu, hayo matetemeko makubwa ya dunia wakati huo yaliitikisa yakaizamisha moja kwa moja majini.

93 Unasema, "Yoyote! Mradi tu ninayo dini, yote yatakuwa shwari." La, sivyo. Haina budi kuwa ni ujuzi uliotokana na Mungu katika dini. Mnaona? Mwingine wote utaangamia. Sisemi hili nipate kuwa tofauti. Ninalisema tu kwa sababu ya

upendo, na nikijua ya kwamba ni—nitawajibika kwenye siku ile, na niwajibike. Kwa hiyo nikisema tu yale Yeye asemayo, basi ninajua yote ni sawa. Lakini nikijaribu kuweka kanuni ya imani ya mtu fulani ama nadharia ndani yake, ni—nisingeweza kufanya hivyo, sina imani yoyote nayo. Ninaamini tu yale Yeye aliyosema.

94 Sasa angalieni, baada ya kitambo kidogo yakapata kilindi zaidi, na hata urefu zaidi. Wakabisha mlangoni, wakapiga mayowe, wakalia. Halikufaa kitu hata kidogo. Labda siku chache hapo kabla, walipowaingiza wanyama mle ndani, ningeweza kuwasikia baadhi ya wenye dhihaka wakisema, "Ingia mle ndani pamoja na wanyama wako wanaonuka. Ishi na uvundo wako wote mle ndani ukitaka."

95 Hiyo ni siku hizi tu, wanakwambia jambo lile lile. "Endelea, kuwa wa mtindo wa kale ukitaka. Sisi tutajifurahisha." Endelea, achilia. Lakini, loo, ndugu, ili kuwa salama katika Safina, mlango ulijifunga! Hilo, jambo ndilo hilo.

96 Lakini Nuhu, katika siku zake, ilikuwa ni vigumu kwake katika kipindi chake cha wakati, mnaona, kwa sababu kuwa watu kamwe hawakuwa wamesikia kitu kama hicho, bali kilitokea haidhuru. Ndipo tunaona jukwaani, kikaja baada ya ukombozi wa Nuhu na kadhalika, ndipo ulimwengu ukaanza kukua tena, na—na kila kitu kilichokuwa na pumzi kikafa. Ndipo basi tunaona tena kwamba kulikuja wakati, basi, Mungu alikuwa akiwatoa watoto Wake Misri, kwamba Musa alijitokeza pamoja na torati. Ilikuwa ni vigumu sana kwa watu kuelewa, bali kipindi cha wakati kilikuwa kikibadilika kuwa torati. Ndipo baada ya torati kuja, Musa akijaribu. . .Ilikuwa ni mwalimu. Watu walikuwa wakiishi tu vyovyote walivyotaka, kwa hiyo mwalimu, ile torati, ilikuwa, Biblia ilisema, kuwaleta watu watambue ya kwamba ilikuwa ni kosa, kwa hiyo Yeye akawapa zile Amri Kumi. Lilikuwa ni badiliko kubwa, hao watu hawakutaka kuzipokea. Vema.

97 Ndipo baada ya Musa, akaja Yohana. Na baada ya Yohana, kile kipindi cha wakati kikaja, akamtambulisha Yesu. Ndipo Yesu alipokuja kujaribu kutuletea neema, ambayo ilikuwa ni Mungu katika Roho, kulingana na Roho, akaudhihirisha upendo Wake, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee," naye Yesu alikuwa tofauti sana na kinyume na torati, mnaona, bali kilikuwa ni kipindi kingine cha wakati, wakati mwingine.

98 Ndipo basi Yesu alipoondoka, alinena juu ya kipindi hiki cha wakati wa Roho Mtakatifu, Uzima wa ndani, Shahidi Wake wa ufufuo. Ninayo Maandiko mengi hapa, bali kamwe sina wakati wa kuyaendea, nitayapitia tu kifupi. Vema. Daima imekuwa ni jambo la hakika na vi—vita, hapo kipindi kimoja cha wakati kinapobadilika kutoka kwenye kipindi cha zamani kuingia kwenye Ujumbe wa wakati huo, daima imekuwa ni vita

na watu. Wao—wao—wao. . .Ni, ingawa sikuzote kimekuwa ni cha Kimaandiko. Lakini kwenye wakati ambao Mungu huwapa kipindi cha wakati na kitu fulani cha kuishia, ama jambo fulani la kufanya. Sasa tunaona kwamba mara baada ya kipindi hicho cha wakati kutolewa, watu wa duniani hujaribu kupata kitu fulani cha kupinga hicho, na kitu fulani cha kufanya jambo la kubuniwa na wanadamu.

99 Nuhu akiisha kuwa na ile safina, ndipo basi mara baada ya hapo, Nimrodi, yule haini, alijenga mnara, na kusema, "Iwapo mafuriko yatakuja, tutapanda tu juu na kuwa juu yake." Ndipo Mungu akaja kule na torati ambayo ilininii tu. . .Mnaona, kipindi hicho cha wakati kilikuwa kimeuishia wakati wake.

100 Ndipo Yesu alipokuja, pia, baada ya torati, torati ilinena juu ya Musa na. . .ilinena juu ya kuja kwa Kristo. Bali hapo Yeye alipokuja, walikuwa wamezama sana katika mapokeo ya baba zao, walikuwa na kanuni zao za imani, walikuwa na mitindo yao, walikuwa na makanisa yao, walikuwa wametulia, kwa hiyo ilikuwa ni vigumu sana kwa Yesu kujaribu kuutikisa ufalme huo (kanisa hilo) kutoka kwenye kanuni za imani, wapate kumwamini Yeye. Na hata hivyo Maandiko hasa yalinena juu ya Mtu huyu kote kutoka kipindi cha kwanza cha wakati cha Edeni, "Uzao Wake utakiponda kichwa cha nyoka." Yalimwahidi Yesu kupitia kila kimoja cha hivyo vipindi vya nyakati, na, hapo Yeye alipokuja, hawakumtambua, kwa sababu walikuwa wamefungwa sana katika kanuni zao za imani. Lakini hata hivyo ilikuwa ni kweli ya Kimaandiko. Kila mjumbe na Ujumbe wake alitabiri juu ya yule atakayefuata, kila wakati. Musa, manabii walitabiri, Musa alitabiri juu ya kuja kwa Yesu. Musa alisema, "Bwana Mungu wako atawainulia Nabii kama nilivyo mimi." Ni mara ngapi tumepitia hilo katika Jumbe zetu kote ulimwenguni, kwamba Masihi ajaye alikuwa awe ni Nabii!

101 Hiyo ndiyo sababu yule mwanamke mwenye sifa mbaya, dhidi ya wahudumu wote, yeye aliamini Ujumbe. Yule mwanamke kule Samaria, hapo Yesu alipokuwa akisema naye, Yeye alisema, "Nipe maji ninywe."

102 Mwanamke akasema, "Huna kitu cha kuchotea. Si kawaida Wewe kuniomba mimi, mwanamke Msamaria." Nayo mazungumzo yakaendelea.

Kisha Yeye akasema, "Nenda kamwite mumeo mje naye hapa."

Mwanamke akasema, "Sina yeyote."

103 Kasema, "Hiyo ni kweli, unao watano, na yule unayeishi naye sasa si wako."

104 Akasema, "Bwana, naona ya kwamba Wewe ni Nabii. Sasa, tunajua ya kwamba kunakuja badiliko la kipindi cha wakati. Yuaja Mtu Ambaye atatiwa mafuta, anayeitwa Masihi, Kristo wa Mungu, basi, ajapo, Yeye atakuwa ndiye yule

Nabii." Ni mengi zaidi jinsi gani mwanamke huyo aliyojua kuliko wahubiri wote wa siku hiyo! Naam. Naye katika hali yake, mnaona, aliyafahamu Maandiko. Hata hivyo, maskini mwanamke, aliyeolewa na wanaume watano, huku akiishi na wa sita, na hata hivyo alijua zaidi kuyahusu Maandiko, kwa sababu aliyachukua jinsi yalivyokuwa. Naye akasema, "Ajapo, atakuwa ni Nabii."

Yesu alimwambiaje? "Mimi Ndiye."

105 Basi akaacha mtungi wake wa maji akakimbia mjini, kasema, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyo kuwa ndiye Masihi?" Mnaona? Huyo Ndiye.

106 Sasa, mnaona, a—alijua Yeye alikuwa yuaja, kwa sababu manabii na Maandiko yalikuwa, katika siku za Musa, na katika siku za manabii, na kote kote katika kila moja ya vipindi hivyo vya wakati, yalikuwa yamesema, "Atakuwa hapa, na hivi ndivyo atakavyokuwa!" Loo, jamani!

107 Laiti watu wangaliweza tu kuona hilo leo hii, basi wangejua siku tunayoishi. Wangeona ni ahadi ya Mungu kwa ajili ya siku hii. Mungu alisema ingekuwa hivi. Hakuna chochote kibaya, saa kuu ya Mungu inapiga tu vizuri hasa. Na, hata kulingana na sayansi, ni usiku wa manane kasoro dakika tatu. Kwa hiyo, mnaona, lile pigo linaweza kutokea wakati wowote. Na hiyo imekuwa ni miaka miwili ama mitatu iliyopita tangu waliposema hivyo. Mnaona, tuko katika wakati wa mwisho. Lakini, mnaona, tumebadilisha vipindi vya nyakati kutoka kwenye ule wakati wa zamani wa kanisa wa huku nyuma ambako siku ile yenye huzuni ilikuwa, kujiunga tu na kanisa na kuandika jina lako kwenye kitabu; hata kwenye Nuru ya jioni, kule kurejeshwa, kurudi tena kwa Roho Mtakatifu juu ya nchi, pentekoste nyingine, ishara nyingine, kitu kingine kilichokuwa kitukie. Wala watu hawaliamini Hilo, kwa sababu ni wakakamavu sana kama walivyokuwa katika siku za Yesu. Mnaona? Yeye alinena juu ya siku hii. Wakati Yeye alipokuwa hapa duniani, Yeye alikuja kulingana na Maandiko kabisa; kisha akatabiri juu ya kuja kwa siku *hii*.

108 Sasa, sasa tunataka kuwazia juu ya mwingine hapa. Ninayo. . .Mkitaka kusoma baadhi yake, Mathayo 24. Yesu alinena habari za siku hii, Yeye alisema Wayahudi watakusanyika tena katika siku za mwisho. Alisema, "Mwonapo mtini ukichipuza majani yake, basi jueni wakati umekaribia." Akasema, "Kutakuwako na mshangao wa wakati, dhiki kati ya mataifa, bahari ikinguruma; mioyo ya wanaume ikivunjika kwa ugonjwa wa moyo, kila mara." Sio miongoni mwa wanawake, sasa. Ni miongoni mwa wanaume. Yesu kamwe hakusema wanawake; "wanaume." Angalieni hiyo tauni! Na katika siku hiyo yale yatakayotimia! Hiyo itakuwa ndiyo ishara ya wakati wa mwisho, "Mioyo ikivunjika, hofu, mshangao." Ufunuo, Huo uliponena, huyo nabii akinena juu ya siku hii, yeye alisema ya

kwamba ungekuja wakati ambapo kanisa lingekuwa vuguvugu, Wakati wa Kanisa la Laodikia katika siku za mwisho. Mnaona? Ni kitu gani? Ni Yesu (ule wakati wa mwisho) akibashiri mwisho wa wakati huu.

109 Sawa kabisa na Edeni, sawa na wakati wa Nuhu, na chini katika wakati wa Musa, chini katika wakati wa torati—torati, halafu wakati wa neema, na sasa katika wakati wa jioni. Kuna vingine vingi mle kama tu—tungalikuwa na wakati, bali nimeviruka tu maana hatutakuwa na wakati. Wa kila mmoja akisema kile kingekuwako katika wakati ufuatao, bali kanisa linakuwa la kikanisa sana pamoja na kanuni zao za imani, pamoja na mafundisho yao ya sharti, na imani zao za kujifanya na nadharia zao zilizobuniwa na wanadamu, mpaka wanalikosa Neno lile. Sasa mnaweza kuona kile uinjilisti wa wakati wa mwisho utakachokuwa. Mnaona? Ni kitu gani? Wale watakaoutekeleza wataitwa wenye kichaa. Watakuwa tofauti sana! Walikuwako katika wakati wa Nuhu, walikuwako katika kila wakati. Wakafukuzwa makanisani mwao kwa sababu walimwamini Yesu, yeyote aliyemsikiliza ilibidi atupwe nje ya kanisa lao. Mnaona? Lakini Yeye alikuwa na kipindi hicho cha wakati, huo ulikuwa ndio wakati Wake, kipindi cha wakati cha Mwana.

110 Sasa, tunaona pia ya kwamba Roho Mtakatifu mkuu alitabiri juu ya hilo. Ukitaka kuandika baadhi ya Maandiko haya, Mathayo 24, kisha uandike Timotheo wa Pili 3:1. Roho Mtakatifu ananena juu ya wakati mkuu wa kiakili kwenye wakati wa mwisho. Mlijua hilo? Mbona hivyo?

111 Joseph, umesafiri pamoja nami sana humu nchini na umesikia juu ya mikutano katika nchi za ng'ambo. Ninaenda katika nchi za ng'ambo na kuwa na mia moja na hamsini, mia mbili elfu, elfu mia tano, nao watu wananinii tu. . .Jambo moja tu, unaloliona likifanywa kila siku, kwamba mikutano inaendelea, karibu hivyo, hapa maskanini; kufikia watu elfu kumi, ishirini na thelathini wataanguka miguuni mwao. . . kutoka miguuni mwao, kumpa Mungu sifa. Wanaliona Hilo. Kuna shida gani, halifanyiki Marekani? Ni wakati wa kiakili. Wanamtaka mtu ambaye anaweza kuzungumza sio juu ya hukumu, sio juu ya mambo haya, kwa sababu yanawavunjia ushirika wao pamoja na vilabu vyao na—na vyama vyao, na—na kazi za upotevu wanazoshiriki. Kwa hiyo, kama mchungaji wao angetaja kitu kama hiki, halmashauri ya mashemasi ingemwondosha mamlakani, na kumweka mtu mwingine, riki fulani mdogo ama kitu fulani. Mnajua ninalomaanisha.

112 Mimi. . .Samahani hilo, mnaona, si—sikumaanisha hilo, mnaona, bali wakati mwingine ninachochewa kupita kiasi, nadhani. Lakini ninamaanisha. . .Riki ni sawa. Ni kwamba tu silipendi jina hilo, hiyo ni kweli. Lakini wewe liangalie hilo katika numerali, ungempa mtoto wako jina lingine. Naam,

bwana. Sasa, Riki ama Elvis, ama kitu kama hicho, loo, rehema! Kwa hiyo, loo, vyovyote vile, sasa, unaona inawabidi kufanya hivyo. Hawakuwa na majina hayo siku zilizopita, hauna budi kuja. Huu ndio wakati wake wa kuwa hapa. Hakika. Kweli kabisa.

113 Sasa, "Na sasa Roho ananena." Sasa sikilizeni, ninawanukulia kutoka kwenye Maandiko.

> *Sasa Roho* ananena waziwazi, *kwamba wakati wa mwisho,* mnaona, *wakati wa mwisho watu watajitenga na imani*, *wakisikiliza roho zidanganyazo,* . . . *mafundisho ya mashetani;* na kadhalika, mnaona.

114 Angalieni jinsi wangekuwa, "Wakaidi, wenye kujivuna," watu wazito. Samahani kwa hilo, bali mnajua wale tunaowaita wazito, msamiati wa mtaani sasa. Sote tunajua vema kuliko kusema namna hiyo. "Wenye kiburi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu."

115 Nilisimama pale jana, nikaangalia kile kidimbwi cha kuogelea papo hapo chini yetu. Ndipo, nikashangaa, wakati mtu, ambaye ni mwalimu wa shule ya Jumapili, aliponiambia, "Hapo hapapaswi kuwa kwenye Biblia, ambapo Yesu alitema mate." Kasema, "Ni kukiuka masharti ya afya wakati Yesu alipotema mate na kufanya, alipochukua mate Yake."

116 Alikuwa amesimama, akizungumza, Kiyunani asilia kilisema "Alikuwa akitema mate ardhini." Akizungumza na mtu huyu, huku anatema mate ardhini. Alipomaliza, alichukua mkono Wake, akaunyosha mkono, akachukua hayo mate pamoja na matope akayasugulia machoni mwake, akayapaka kwenye macho yake, na kusema, "Nenda, kanawe kwenye birika la Siloamu (akamtuma) nayo macho yako yatafunguka." Naye akaenda akanawa, macho yake yakafunguka.

117 Kwa hiyo jamaa huyu akaniambia, "Hilo lisingefanya kazi leo hii. Hilo ni kinyume na kanuni ya usafi, kanuni za afya." Kisha mtu yuyo huyo anaipeleka familia yake, mke na watoto hao wote kule chini kwenye kidimbwi hicho cha kuogelea ambako wanawake hao wote na wanaume, huku wakiwa katika maji hayo nyakati za mwezi ambazo haiwapasi kuwamo, na yote hayo. Hawaendi msalani wakati mwingine, na—na hiyo miili yote michafu na takataka mle ndani, nao huku wanayatema kupitia vinywani mwao, na machoni, na vitu kama hivyo. Kisha useme kwamba Yesu kutema mate ardhini na kumfanya mtu kuona!

118 Nilimleta mvulana mdogo kutoka huko hivi majuzi, akasema, "Nilimeza baadhi ya maji hayo," kasema, "mimi ni mgonjwa kama farasi. Ni—ninaenda nyumbani." Maskini jamaa huyo huenda ameketi hapa sasa, anayeishi kwenye trela yapata majengo mawili au matatu chini mtaani, ambapo nilimchukua, akasema, "Kamwe sitaingia mle tena."

119 Lakini hata hivyo huo unaitwa "ustaarabu wa kisasa." Mnaona mahali mnapofikia? Ule msemo wa kale wa "kukabwa na mbu na kumeza ngamia," mnaona. Nina shauku tu ya kukutana naye sasa. Sasa, haya basi. Heri myaondokee mambo hayo, mnaona.

120 Mwenye akili, "wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu." Ninayanukuu Maandiko. Roho Mtakatifu ananena waziwazi kwamba hili lingetukia katika wakati wa mwisho. "Wakaidi, wenye kujivuna, wenye mfano wa utau-. . ." Vema, kwanza, "Watakuwa wasiojizuia, wasiowapenda walio sawa," wenye kuwachukia wale wanaoliamini Neno. Mnawaona? Hawakubaliani na kanuni hizi za imani za mapokeo na kadhalika, kwa hiyo wanawachukia.

121 Kama wale Mafarisayo na Masadukayo, walimchukia Yesu. Kwa nini? Kwa sababu Yeye alikuwa—Yeye alikuwa akikanusha kanuni zao za imani. Mnaona? Sio kwamba alitaka kuwa tofauti, bali, Yeye hana budi kuishi, Yeye alikuwa Neno, Neno lililo hai. Akasema, "Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini." Mnaona?

122 Vema, jambo lile lile siku hizi. Kama mtu akiyahubiri mambo haya, nayo hayatendeki, basi ni makosa, kwa kuwa Maandiko yalisema yangetendeka. Ndipo yakitukia, basi hiyo ni kweli; sio kwamba mtu huyo ni sahihi, bali hilo Neno ni sahihi. Sasa, bali hii ndiyo hali tuliyoingia leo hii. Mnaona, marafiki, ni la maana tu hivyo. Mnaona jambo hilo? Ninajenga hapa kuwaonyesha upeo hapa kwenye uinjilisti wa wakati wa mwisho.

123 Sasa angalieni katika nyakati hizi, wakati wa kiakili, "Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu," wanakaa nyumbani Jumatano usiku kuangalia baadhi ya maskini michezo hiyo ya kishenzi, "Tunampenda Susie," ama "Lucy," ama upuuzi huo wote ulicho, mwanamke aliyeolewa mara dazani moja na anaishi na mwanamume, nao wakiishi . . . Na, loo, jamani, kila mmoja wao ameolewa na kutalikiwa, na kuolewa na kutalikiwa, nanyi mnawafanya sanamu, kama miungu. Lakini afadhali ukae na kuuangalia huo kuliko kuhudhuria mkutano wa maombi. "Wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu." Acha mchezo wa mpira uingie mjini, ama Makanali na Majitu, ama wowote waliojiri kukutana hapa nje mahali fulani, wanafunga makanisa wapate kuihudhuria. Acha Elvis Presley ashuke aje hapa mtaani, pamoja na gita yake, aanze kuipembeza mbele na nyuma, ama baadhi ya jamaa hao, Jumatano usiku, mikutano ya maombi ingefungwa. "Wenye kupenda anasa kuliko kumpenda Mungu. Wakaidi, wenye kujivuna, wasiojizuia, wakali, na wasiowapenda walio wema. Wenye mfano wa utauwa!"

Mnasema, "Hao ni Wakomunisti." La, sivyo.

124 Hao ni wafuasi wa kanisa, wenye mfano wa utauwa. Lakini nini? Wakizikana Nguvu zake! Wenye mfano wa Mungu, bali wasema, "Mungu hafanyi mambo haya. Mnaona, hamna Nguvu kwake, mnakubali tu na kufanya *hivi*, *vile*." Mnaona, hakuna mabadiliko ya maisha, hakuna chochote, ni ku—kuwa tu mfuasi wa kanisa.

125 "Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake. Hao nao ujiepushe nao," Biblia ilisema. "Kwa maana hawa ndio wajiingizao nyumba kwa nyumba, na kuwaongoza wanawake wajinga wenye mizigo ya dhambi, waliochukuliwa mateka na tamaa za namna mbalimbali." Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema hasa. Sasa tunaishi katika wakati huo hasa. "Lakini wewe fanya kazi ya mwinjilisti, fanya thibitisho kamili la huduma yako." Mnaona, jambo ndilo hilo.

126 Sasa, kwa njia ya wajumbe hawa na mashahidi tunaowaona, tunaona tuko kwenye zao lipi. Angalia uko kwenye zao lipi asubuhi ya leo. Angalieni tuko kwenye zao lipi. Mbona, Yeye alisema, upande *huu*, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, watafanyiwa mizaha na kudhihakiwa kama siku za Nuhu. Na *hapa* litakuja kundi hili lingine hapa nyuma likiwadhihaki, wakaidi, wenye kujivuna, na wenye mfano wa utauwa, bali wakikana kile kitu chenyewe mnachokiri. Kwa hiyo mnaweza—mnaweza kuona mko kwenye zao lipi, mnaona, wajumbe hawa wa kweli wa siku hizi! Yesu alitabiri kwamba *huyo* angekuwa ni Shetani na ujumbe wake. Naye mjumbe Wake angekuwa akiliendeleza *hili*, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Mnaona, wajumbe wa Shetani watakuwa na mfano wa utauwa. Wajumbe Wake watakuwa na ishara hizi, kuchukua nyoka, kunywa vitu vya kufisha, kuwatoa pepo, kuweka mikono juu ya wagonjwa, kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, ishara na maajabu. Sasa, tuko katika moja ya hayo mazao, nasi tuko katika wakati wa mwisho. Loo, jamani!

127 Si ajabu nabii Isaya alisema, "Mwili wote umeoza na umejaa vidonda vitokavyo usaha, kila kitu." Twende wapi? Tungefanya nini kama sote tungeungana pamoja? Lingekuwa baya zaidi kuliko hapo awali, mnaona, kungekuwa na kila namna ya mambo. Kama wanavyolijaribu Ba—Baraza La Makanisa Ulimwenguni, kamwe halitafanikiwa, wanao makafiri, wasioamini. "Basi wanawezaje—wanawezaje wawili kutembea pamoja," Biblia ilisema, "wasipopatana?" Mnaona? Wala hamna wawili wao watakaokubaliana pamoja.

128 Wokovu ni jambo la mtu binafsi kati ya, si kanisa, bali kati ya kila mtu binafsi na Mungu. Kutembea pamoja na Neno! Naam. Angalia, ndugu, tunapoona. Nami najua ninachelewa sana.

129 Angalia, kile kimulimuli kikuu chekundu cha dalili ya Kuja Kwake kimeshushwa. Tunajua hilo. Ningeweza tu kuchukua Maandiko mengi hapa niliyoandika chini kuwaonyesha, kile, tuko katika wakati wa mwisho. Wayahudi wamerudi Palestina,

mtini umechipuza majani yake. Mioyo ya watu inavunjika kwa hofu. Wanawake, ghasia walimo ndani yake, jinsi ningerudi kwenye Ufunuo na kuwaonyesha taifa hili hapa limetiwa alama na wanawake, namba ya mwanamke, namba kumi na tatu. Tunazo, kwa kuanzia, koloni kumi na tatu, milia kumi na mitatu, kila kitu ni kumi na tatu, majimbo kumi na matatu, kila kitu, kumi na tatu, nyota kumi na tatu kwenye dola, kila kitu ni kumi na tatu na mwanamke.

130 Niliposimama si muda mrefu uliopita huko Uswisi, nami nilikuwa nikizungumza. Mwanamke mmoja alisema, "Mimi, sisi tunataka kuja huko Marekani tupate uhuru kama wanawake wa huko." Nikawaambia yale waliyofanya. "La," wakasema, "hatuyataki hayo, basi." Mnaona? Mnaona?

131 Lakini ni Marekani. Tungeweza kurudi nyuma na kulionyesha hilo papa hapa, kwamba hilo linapaswa kuwa katika taifa hili linalotokea ambapo hamna maji, hamna watu. Linatokea kama mwana-kondoo, linazo pembe mbili ndogo, nguvu za kisiasa na za kidini, bali zinaungana pamoja kupitia nguvu za kisiasa, Rais mpya tuliye naye, akiingiza Rumi tena.

132 Ninataka mtu yeyote aniambie, mwanatheolojia yeyote hapa ama mahali popote pengine, ambapo Biblia kamwe inabashiri kwamba Ukomunisti utautawala ulimwengu. Msiogope Ukomunisti, hauna kitu. Ni kitu cha bandia ambacho Mungu anakitumia kuyaadhibu mataifa kwake, kulicharaza taifa. Hakika. Biblia inasema Rumi itautawala ulimwengu. Mwangalie Mfalme Nebukadreza, ndoto yake, ono lake, fasiri ya Danieli, jinsi kila moja ya falme hizo na vipindi vya nyakati vilivyotimia kikamilifu, na moja kwa moja pale mwishoni kulikuwako na Rumi. Kwa hiyo, itakuwa ni Rumi. Haitakuwa ni Ukomunisti, hao ni ninii tu—hao ni vibaraka tu. Hivyo tu. Kamwe hawataenda popote. La, hawataenda.

133 Kama vile Joseph ndio kwanza aseme, "Moyo wa Afrika, hao makafiri maskini huko nyuma hawatatawaliwa. Tayari wametawaliwa." Hiyo ndiyo shida yao siku hizi, wametawaliwa. Wanataka upendo, wanamtaka Mungu. Basi wakati Ukomunisti ni ukafiri, basi kamwe hawataukubali huo. Bila shaka hawataukubali, la hasha.

134 Taa nyekundu inamulika. Selo imeshushwa. Kuja Kwake kumekaribia. Loo, jamani! Isaya, mlango wa 60 na kifungu cha 2, ilisema, "Giza litaifunika dunia, na giza kuu litawafunika watu." Na hiyo ni kweli kabisa.

135 Mjumbe wa wakati wa mwisho na Ujumbe wanapaswa kutimiza masharti ya wakati wa mwisho. Mwaonaje? Ujumbe huu usingalihubiriwa miaka arobaini iliyopita. La, Ujumbe wa wakati wa mwisho na mjumbe wake hawana budi kukutana. Huko nyuma katika siku hizo walizokuwa nazo, labda usingefanya kazi. Lakini hauna budi kuendana na masharti

ya wakati wa mwisho. Ongokeni, ziaminini ishara za Injili! Huo ndio Ujumbe wa leo hii. Ziosheni nafsi zenu katika Damu ya Mwana-kondoo na muiamini Injili, kwamba zile ishara za wakati wa mwisho zimewadia, mbegu ya Injili imekuwa ikitukia.

136 Wanazungumza sana juu ya matengenezo, nitaambatana nao juu ya hilo, kama vile matengenezo ya kiinjilisti. *Matengenezo* maana yake ni "kutakaswa kabisa." Kwa hiyo nafikiri tunahitaji utakaso mwingi, wa kutokuamini kwetu, na kuiamini Injili. Hiyo ni kweli. Tuhuma zetu nyingi kupindukia na maajabu. Matengenezo! Hata neno la kawaida katika fasiri ya Kiyunani linalosema *tubu,* lenyewe linamaanisha "kutengeneza." Nako *kutengeneza* kunamaanisha "kutakasa kabisa," kote nyuma, yaliyopita, na kuiamini Injili katika nguvu Zake na madhihirisho. "Ishara hizi zitafuatana na hao."

Wao wanasema, "Kwa wakati huo pekee."

137 Yeye alisema, "Hata ukamilifu wa dahari." Sasa, mtu fulani anasema kweli. Endapo mtu ambaye haamini alisema ya kwamba hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya mitume pekee, naye Yesu Mwenyewe alisema "hata ukamilifu wa dahari," basi ninachukua Neno Lake kwa ajili yake. Hilo ni, Hilo ni kweli!

138 Mungu anawataka watu Wake watengwe na kutokuamini na wasioamini. Wengi wenu nyinyi watu hufanya kosa katika jambo hili, wakati mwingine mkiwaacha watoto wenu wacheze hapa nje mtoto Oswald. Mnaona? Simaanishi kuwa tofauti sasa, na mgumu, na kadhalika, na kuwa namna fulani ya mshupavu. Simaanishi hilo. Lakini mkimwacha. . . Wewe kuwa na hakika ni nani binti yako anatoka kwenda naye usiku. Mnaona? Labda ulimlea maskini msichana mdogo mtauwa kanisani, na muda si muda wajua anatoka kwenda pamoja na Oswald ama baadhi yao, na—naye ni kafiri, asiyeamini, basi maisha yake yataangamizwa wala hujui yeye ni nini. Unaona? Ndipo atamwoa, basi angalia mahali watoto wako waliko, wajukuu wako, basi, unaona. Kuwa mwangalifu. Mungu anawataka watu Wake watengwe.

139 Hebu soma Kutoka 34:12 wakati mmoja, uone yale Mungu aliyowaambia Israeli. "Mnapokwenda kwenye nchi hiyo, fagilieni mbali kila kitu kilicho kule. Msiwe na uhusiano wowote nacho." Yoshua pia, mlango wa 23 na kifungu cha 12, angalieni yale Yoshua aliyosema, "Sasa Mungu amewaleta kwenye nchi hii nzuri," kama vile Kanisa sasa, "akawaleta kwenye nchi hii nzuri. Mnaifurahia?"

Wakasema, "Amina, tunaifurahia."

140 Kasema, "Sasa kuna masalio, hawa wasioamini hapa nje, na kamwe msishirikiane nao. Msiende pamoja nao." Usifanye hivyo, dada, kama mvulana huyo anataka kukupeleka kwenye baa mahali fulani, kupata tu kinywaji kidogo cha kirafiki, kaa

mbali naye! Na jambo lile lile, ninyi wavulana, kwa msichana huyo ambaye angefanya jambo lile lile. Kaeni mbali nao!

141 Sasa mtasema, “Ndugu Branham ni mzee mwenye kichaa.” Lakini moja ya siku hizi mtajua. Kama ungalipitia kwenye njia ambayo nimepitia, unge—ungejua kwamba hiyo ni kweli. Naam, bwana.

142 Ni mara ngapi nimeona, kwenye vyumba vya maungamo, ambako wasichana wadogo wangekuja katika—katika aibu. Alama hiyo itaambatana naye mpaka atakapokufa, na mambo aliyosema: Wakati mmoja alilelewa kwenye makazi ya Kikristo, lakini hili hapa lililotukia, alitoka akaambatana na mvulana huyu. Alikuwa mzuri sana wa sura msichana asingeweza kumwacha, na—na yote namna hii. Na, jambo la kwanza, mvulana akavuta sigara na alikuwa na chupa mfukoni mwake, nao wakaanza kunywa, nawe huyu hapa. Mnaona? Naye huyo hapo katika aibu na hayo. Loo, ni jambo la kusikitisha. Unaliona pande zote mbili. Kwa hiyo kaa tu mbali, jitenge! Kuwa mzuri na mwema kwa kila mtu, bali usishiriki dhambi yao. Kaa mbali nayo. Naam, bwana.

143 Na sikuzote, enyi marafiki, viongozi, kila wakati kote katika badiliko la vipindi hivi vya nyakati, wamewavuruga watu kabisa. Sana sana haijakuwa ni hao watu, kama Injili ingalikaa mimbarani mahali Pake!

144 Kama vile nilivyokuwa nikizungumza na Chuo cha Bethany kule, wale Walutheri. Yeye alisema, “Ndugu Branham, unafikiri sisi tuna nini?” Nami . . . yeye akasema . . .

Nikasema, “Vema, jambo ndilo hili.”

145 Akasema, “Tofauti kati ya pentekoste hii unayonena habari zake na sisi Walutheri ni ipi?”

146 Nikasema, “Kanisa la Kipentekoste ni kanisa la Kilutheri lililoendelea mbele. Hiyo ni kweli kabisa. Kama mngalikaa mahali mlipopaswa kuwa, mngalikuwa Pentekoste pia.”

147 Nasi sote tunazungumzia kama nilivyomsikia mtu fulani akisema asubuhi ya leo, ya kwamba “Makanisa yote, dini yote—yote ya kwanza, Wakristo wote kweli walitoka Rumi.” Ninataka mtu fulani anithibitishie hilo. Nitakubali madhehebu yote yalitoka Rumi. Bali Wakristo walianzia Yerusalemu.

148 Kwa hiyo iwapo ukasisi wa Katoliki unatutaka sisi sote turudi kwenye mama wa Ukristo, nitakubaliana naye kwamba, hebu turudi Pentekoste na sote tumpokee Roho Mtakatifu. Nitakubaliana naye hapo. Kwamba, kamwe haukutoka Rumi, Huo ulitoka Pentekoste. Kanisa halikuanzishwa katika Rumi, lilianzishwa kwenye Siku ya Pentekoste. Hakika, sio chini ya mafundisho yao ya sharti, bali chini ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hilo ndilo ninalojaribu kusema. Kama tukirudi, hebu turudini mwanzoni mwake; sio kurudi kwenye dhehebu,

mnaenda Rumi, maana walikuwa wa kwanza waliokuwa na shirika ama dhehebu, nalo ni mama wa hayo yote.

149 Nayo Biblia ilisema hivyo, katika Ufunuo 17, "Yeye ni kahaba, yeye mwenyewe, na mama wa makahaba, binti zake." Mnaona? Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Yesu Kristo alisema hivyo, "Kwamba kanisa Katoliki la Kirumi lilikuwa ni kahaba, na binti zake wote wa Kiprotestanti walikuwa ni makahaba pamoja naye." Naye alisema, "Tokeni miongoni mwao, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake; nami nitawapokea, nanyi mtakuwa wana na binti Kwangu." Mnaona? Kwa hiyo haya basi, mnaona, "Wenye mifano ya utauwa, na kukana Nguvu zake," na kadhalika.

150 Ninyi Wamethodisti wa thamani, jinsi mlivyokuwa na nguvu za Mungu miongoni mwenu. Nilienda na kusimama . . . Nilivaa joho la John nilipokuwa London, Uingereza, kumwombea Mfalme George wakati huo. Nao wakanipeleka kule kwenye Kanisa la Wesley ambamo aliwahubiri elfu moja na mia tano kila asubuhi saa kumi na moja, kabla hao watu hawajaenda kazini. Nikaketi hapo kwenye kiti ambamo alimwongoa mpiganaji huyu wa jimbi, na mimi—mimi nikaketi kwenye kiti hicho. Ndipo nikasimama pale, na kwenda kwenye mimbara yake. Nikaombea humo chumbani ambamo aliendea Mbinguni. Nikawaza, "Loo, laiti John angalijua yale kanisa hilo la Methodisti limefanya, angalipinduka kaburini mwake." Wakati mlikuwa mkiwaombea wagonjwa na kuwa na ishara kuu! Wakati John Wesley . . . akisimama huko nje, yale madhabahu niliyosimama karibu nayo, ambapo pana mti. Siku hiyo, akihubiri uponyaji wa Kiungu, nalo ka—kanisa kuu la Uingereza, kanisa la Kianglikana, likaenda na kuwafungulia . . . Kundi la wafuasi likashuka pale na kumfungulia mbweha na kundi la mbwa wakubwa wawindaji, na kulitawanya kusanyiko la John. Maskini John kamwe hakuwa na uzito wa zaidi ya pauni mia moja na kumi wakati wowote maishani mwake, bali aligeuka na kuelekeza vidole vyake, na kusema, "Ewe mnafiki! Jua halitatua juu ya kichwa chako mara tatu hata utakaponiita nikuombee." Naye akafa jioni hiyo, akiwa na mkakamao wa misuli mwilini mwake, akimwita John aje amwombee. Naye akafa. Mnaona? Loo, kama ninyi Methodisti mngalikuwa Wamethodisti namna hiyo, mngekuwa Pentekoste. Hiyo ni kweli.

151 Vipi kuhusu ninyi Wabaptisti? Mnakimbia kwenda kanisani kwa dakika chache, naye mchungaji akihubiri zaidi ya dakika kumi na tano mnataka kumwondosha. John Smith, mwanzilishi wa kanisa la Baptisti, aliomba usiku kucha wakati mwingine, na kuzililia dhambi za watu mpaka macho yake yangefungika kutokana na kulia, naye mke wake angemwongoza mezani na kumlisha kwa kijiko, kiamshakinywa chake. Hamwezi kuomba dakika kumi na tano tena. Kuna shida gani? Mnaona, mmelichanganya na mapokeo.

152 Ujumbe ungali unaendelea. Israeli waliifuata ile Nguzo ya Moto. Mahali iliposimama, walisimama. Mahali ilipoenda, walienda. Nguzo ya Moto inasonga mbele. Naam.

153 Sasa tunaona ya kwamba ni viongozi wanaosababisha jambo hilo. Viongozi daima wamevurugika. Mwangalieni maskini Dathani huko nyuma katika wakati wa Biblia, katika kipindi cha wakati wa Musa cha torati. Yeye ndiye aliyeliongoza kundi kubwa la watu waliochangamana, Dathani, ilikuwa ni Kora; wakati Mungu alipomwinua nabii Wake Musa, naye alikuwa na Neno la Bwana. Alikuwa na watu milioni mbili na nusu huko nje jangwani, naye Jethro akaja na kusema, "Musa, itakuua, mzigo wako ni mkubwa mno." Mungu akachukua sehemu ya Roho Yake na kuiweka juu ya wazee sabini, nao wakatabiri. Halikumdhoofisha Musa hata kidogo. Yeye, lakini Musa alikuwa angali ndiye jibu la mwisho, maana alikuwa na BWANA ASEMA HIVI.

154 Huwezi kwenda chini ya kundi la watu. Na—nakataa katakata wakati wowote ambapo—ambapo kamwe, ambapo Mungu aliwahi kutumia kundi la watu. Yeye humtumia mtu mmoja. Hakika. Mtu mmoja kwa wakati mmoja, maana watu wawili wana maoni mawili. Mtu mmoja! Kweli kabisa. Angalieni sasa, kila kipindi cha wakati kimekuwa hivyo, kote kote, imekuwa hivyo kila wakati.

155 Basi hapo alisimama Musa. Nanyi mwajua Kora alisema nini? Yeye alisema, "Mbona, Musa anatenda kana kwamba yeye pekee ndiye anayeweza kuhubiri, yeye ndiye pekee aliye na Ujumbe. Loo, tunajua Nguzo ile ya Moto inaning'inia juu yake, tunajua Nuru ile iko juu yake, tunajua hayo yote, lakini anatenda kana kwamba yeye ndiye pekee aliye na Ujumbe."

156 Yeye hakumaanisha hilo. Hakulimaanisha hivyo. Alikuwa akijaribu kuwasahihisha hao watu. Kuna mawazo mengi kupindukia. Inakubidi kusikiliza kitu fulani. Basi ni jambo gani lililotukia? Mungu alisema, "Jitenge tu naye, maana nitammeza pamoja na kusanyiko lake ardhini." Ndipo ardhi ikafunguka na moto ukatoka, nao wakazama ndani. Mnaona?

157 Waliochangamana, viongozi, viongozi ndio waliosababisha hayo matatizo miongoni mwa watu. Kama sivyo, leo hii tungekuja hapa katika mji huu na kila kanisa na kila kusanyiko lingekusanyika pamoja. Mbona, wangefanya mahali hapa, wangefanya, loo, kila baa ingefungwa. Mbona, mji huu ungekauka sana mpaka ingembidi mwuza pombe haramu kujikakamua nusu saa apate unyevu wa kutosha kutema mate. Yeye. . . Mbona, ingekuwa hivyo! Loo, samahani, sikupaswa kusema hivyo. Ngojeni. Hili, yale ninayomaanisha ni haya, sote tumetawanyika. Ni viongozi. Mungu anaweza kuingia kufanya jambo fulani, nao viongozi wa makundi haya madogo wanahofia kitu fulani kinaenda kupotea, watakaa . . . watawaondoa Kwake, badala ya kuukubali Ujumbe wa Mungu. Ilikuwa ni viongozi,

katika siku za Nuhu. Ilikuwa ni viongozi, katika siku za Musa. Ilikuwa ni viongozi, katika siku za Yesu. Ni viongozi, leo hii katika Roho Mtakatifu. Makundi yaliyochangamana! Wao wanasema, "Loo, acheni wanawake wafanye hivyo. Kwa nini unawakemea?"

158 Kama nilivyosema, ninaamini hapa awali, mtu fulani aliniambia hivi majuzi, maana sikuzote nilikuwa nikijaribu kuwafanya dada zangu walainike. Mnaona, hao—hao ndio shabaha. Wamekuwa ndio shabaha katika kila wakati. Shetani aliwatumia huko nyuma katika bustani ya Edeni, naye aliwatumia kila wakati. Basi wakati Biblia inapoonyesha habari za Marekani na wanawake wake katika siku za mwisho, ndipo ninaanza kuwakemea. Basi mtu fulani alisema, "Ndugu Branham, watu wanakuchukua kama nabii."

Nikasema, "Mimi siye."

159 Akasema, "Bali wanakuchukulia hivyo. Mbona usiwafundishe hao watu jinsi ya kupata karama kubwa za kiroho? Uwafundishe mambo kama wewe... Mungu hukushughulikia, tunajua hilo." Kasema, "Mbona usiwafundishe hao wanawake badala ya sikuzote kuwakatakata?"

160 Nikasema, "Nimewahubiria kwa muda wa miaka thelathini na mmoja, nao wananinii...Ninawezaje kuwafundisha, ninawezaje kuwafundisha aljebra, wakati hata hawajui ABC zao? Mbona hata hawatavumilia na kutenda kama wanawake? Ni kwa nini wanaendelea kufanya yale wafanyayo? Unawezaje kuwafundisha mambo ya kiroho wakati hata hawataamini mambo ya kawaida? Unawezaje kuwafundisha mambo hayo?" Hebu kanisa liifikie milki hiyo, ndipo wanaweza kufundishwa katika milki hiyo jinsi ya kuzipokea karama za Mungu na jinsi ya kuzidhihirisha karama na kadhalika. Lakini Roho Mtakatifu kamwe hataliruhusu lije mpaka moyo huo uko sawa na uko tayari kulipokea.

161 Halafu, Mungu akisimama pale kama shinikizo kubwa. Usihofu kwamba kutakuwa na wengi kupindukia. Huwezi kummaliza Mungu. Ungeweza kuwazia maskini panya yapata urefu *huu*, maskini kijipanya chini ya yale maghala makubwa ya Misri, akisema, "Afadhali nile punje moja ya ngano kwa siku, huenda nikaishiwa kabla ya mavuno yajayo"? Ungeweza kuwazia samaki mdogo yapata urefu *huo*, akiogelea katikati ya bahari, akisema, "Afadhali ninywe maji haya kwa unyimifu, kwa sababu, mwajua, huenda yakakauka siku moja"? Loo, jamani, hiyo ni kujaribu kumaliza wema na rehema za Mungu kwa watu Wake! Yeye anataka kuwabariki. Yeye yuko tayari, Yeye anasukumiza. Ungeweza kuwazia kuyachukua maji yote duniani, bahari zote na kila kitu, na kuyalundika kwenye bomba moja la futi nne na kuliweka kule juu? Presha ingekuwa chini yake, ikijaribu kupata mwanya wa kuvujia yapate kutoka. Hiyo

ni kama presha ya Roho Mtakatifu akijaribu kushuka kwenye kila maisha.

162 Lakini hawatafanya hilo, wanapenda kanuni za imani na kadhalika kuliko wanavyompenda Mungu. Inakubidi kujisalimisha kwa vitu vya ulimwengu, na kumwamini Mungu. Hilo haliwezi kukanushwa, mmeliona mwaka baada ya mwaka, na wakati baada ya wakati. Naye Joseph alisema wakati mmoja, "Halikosei. Haina budi kuwa ni Mungu." Mnaona? Nayo ni ahadi ya Mungu ya siku hii. Sio mimi; mimi siyo ahadi ya Mungu. Mimi ni mwanadamu. Ninazungumza juu ya Roho Wake Mtakatifu aliye hapa. Hiyo ndiyo ahadi ya siku hii, "Mahali popote, mtu yeyote."

163 Sasa, tunaona ya kwamba walikuwa ndio hao. Basi, angalieni, nasi tutachukua kwa mfano, Balaamu. Balaamu, yeye alishuka na kuwafundisha hao watu fundisho lake, nao wakasema, "Sasa angalia, sisi sote ni waaminio, sisi ni—sisi ni watoto wa binti za Lutu, Moabu huko juu." Kasema, "Sisi sote ni sawa." Naye akawavuruga, akasababisha kuoana kimseto. Akawafanya hao wanawake warembo wa Moabu, wajipodoe kwelikweli, na wakashuke waje hapa na kuwaambia hawa wana wa Mungu kwamba wa—walikuwa "wote ni sawa, haidhuru; Mungu ni Mungu wa jamii zote, na kila kitu ni shwari." Naye akawafanya waoane. Ndipo Mungu akachora mstari wa utengano, na kuwaacha waondoke nyumbani mwao na kila kitu. Ilikuwa ni kitu gani? Mnakiona kitu hicho? Yale tu hasa yaliyotukia kule nyuma kabla ya ile gharika, "Wakati wana wa Mungu walipowaona binti za wanadamu, walikuwa ni warembo ukiwaangalia, nao wakawatamani na kujichukulia wake." Mnaona? Jambo lile lile lilitukia pale.

164 Na jambo lile lile sasa! Tena ni jambo lile lile. Mnapaswa kuliona. Kila kizazi kinaelezea yale yatakayotukia kwenye kile kinachofuata. Hili hapa. Tunaliona. Tunajua kwamba ni vile vile, maana Biblia hapa inatangaza ni sawa sasa na ilivyokuwa. Vema. Sasa, na yote hayo yana maana yake, hakika, kwa ajili ya si—siku tunayoishi.

165 Sasa, wi—wito wa siku, yote yanayojalisha miongoni mwa makanisa siku hizi, ni wafuasi. Hayo ndiyo yote wanayotaka ni wafuasi. Sasa, sote tunajua ule msemo wa Kibaptisti katika mwaka wa 1944, walisema, "Tutakuwa na milioni moja zaidi, mwaka wa '44." Tunamjua Ndugu yetu Billy Graham wa thamani, mwenye rehema, tunapaona mahali pake katika Maandiko, mahali anapoelekea, yale afanyayo. Lakini sikuzote ni "ukata shauri, kadha wa kadha walikata shauri." Dhehebu tu, hilo tu ndilo wanalotaka. Mnaona?

166 Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika siku za Yesu, jambo lile lile. Hao si watu wabaya. Walikuwa vipofu. Hivyo tu. Walikuwa vipofu kwa ile Kweli. Yesu aliwaambia hivyo, kasema, "Enyi Mafarisayo vipofu na Masadukayo, yale nyote mfanyayo!" Yeye

alisema mnafanya nini? "Enyi waandishi, Mafarisayo, ninyi ni vipofu!" Hakusema, "Ninyi ni wenye dhambi." Walikuwa ni wenye dhambi, bali kile tunachoita dhambi.

167 Sasa, tunaita dhambi, "Kufanya uzinzi, kuvuta sigara, kusema uongo, kuiba, mambo kama hayo, hayo ni dhambi." Hayo si dhambi. Hayo ni sifa za kutokuamini.

168 Biblia ilisema, "Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari." Kutokuliamini Neno, ni dhambi.

169 Hebu waangalieni watu hao, watakatifu. Mbona, usingeweza kuweka kidole juu yao, kimaadili. Babu yao, na baba wa babu, na baba ya babu ya babu, na baba ya babu ya babu ya babu yao wote walikuwa ni makuhani. Walishika torati na mapokeo ya wazee na baba, kikamilifu tu, kote katika hicho kizazi. Hapakuwapo na lawama moja juu yao. Kama wangalikuwa nayo, wangepigwa mawe. Watu wazuri. Naye Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi!" Kwa nini? Kwa sababu hawakuuona ule Ujumbe, Neno. Yeye alikuwa pale.

170 Nao walisema, "Vema, mtu huyu anajaribu kuyararua-rarua makanisa yetu."

171 Yeye akasema, "Enyi Mafarisayo na Masadukayo vipofu!" Akasema, haya hapa aliyosema, Yeye alisema, "Mtazunguka bahari kumfanya mtu mmoja mwongofu. Yote yale mtakayofanya kwa ajili ya mfuasi mmoja! Ndipo mnapomwingiza kwenye dhehebu lenu, yeye ni mara mbili mwana wa jehanamu kuliko wakati alipokuwa huko nje." Hivyo ndivyo Yesu alivyosema hasa.

172 Na kama kuna chochote kilicho dhalimu na chochote kilicho kiovu, ni kumchukua maskini mfuasi wa kanisa anayetangatanga anayefikiria wao ni bora sana, wala hawawezi kuona chochote ila kwa miwani yao wenyewe. Sikosoi. Lakini, naam, ninakosoa, pia. Na, hiyo ni kweli kabisa. Naye Yesu alisema, "Wewe ni mara mbili mwana wa jehanamu kuliko wakati ulipoanza." Basi tunapoyachukua makanisa, ambamo haidhuru ni wafuasi wangapi mnaowaingiza kwenye kanisa hilo, na kuwaona wakienda kuangalia farasi na mashindano ya farasi, na kusimama hapa nje na wanawake waliovaa kaptura, huku na huku mitaani, na kuimba kwenye kwaya, hilo ndilo jiwe kuu mno la kujikwaa alilopata kuwa nalo mwenye dhambi. Kweli kabisa. Wanawatarajia watu hao wanaojiita Wakristo kuishi maisha maadilifu, kuwa mtu tofauti. Huo ni mfano. Hilo ni jiwe la kujikwaa. Huyo ni mnafiki. Hiyo ni mara kumi mbaya zaidi kuliko ulivyowahi kuwa. Ungekuwa afadhali huko nje jinsi ulivyokuwa.

173 Huo ndio wakati mtu anapokuja, anasema, "Vema, wao hawaishi tofauti na ninavyoishi. Vema, hakika hawaishi. Mimi, mimi ningekuwa mzuri kadiri walivyo wao." Ni jiwe la kujikwaa.

Hiyo ni kweli kabisa. Mnawaona wakisema, vema, mwenye dhambi fulani anakuja na kusema, "Yesu alisema hili hapa."

174 "Aa, hilo halikuwa, kwa kuwa hilo—hilo halimaanishi hivyo. Hilo—hilo, Yeye hakumaanisha hilo papo hapo. Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine." Mbona ewe asiyeamini! Unaona? Kuna shida gani? Unaweka jiwe la kujikwaa njiani mwa mtu huyo.

175 Yesu, ama ninamaanisha katika Zaburi, Daudi alisema, "Usiketi kwenye kiti cha wenye kudhihaki, wala kusimama katika njia ya wakosaji." Mnaona? "Usijiweke katika njia ya wakosaji namna hiyo na kuketi kwenye kiti cha wenye kudhihaki, wanaowadhihaki wenye haki, na kusimama karibu wakisema ulikuwa ni mfano wa utauwa. Bali yeye anayependezwa na sheria za Bwana, yeye anapenda kuzitimiza, atakuwa kama mti ambao umepandwa kandokando ya vijito vya maji. Majani yake hayatanyauka. Na chochote afanyacho kitafanikiwa, kitatimia vivyo hivyo hasa." Hiyo ndiyo aina ya kanisa Mungu analotaka. Viongozi vipofu wa vipofu, wakifanya, katika siku hizi za mwisho, wenye kudhihaki wakija, na kadhalika.

176 Ujumbe wa mwinjilisti wa wakati wa mwisho unatoka katika Malaki 4. Ni kurudishwa. Ujumbe na mjumbe, wote wawili, itabidi uwe ni kurejeshwa kwa Imani. Yuda alisema, katika Kitabu cha Yuda, yapata tu miaka thelathini baada ya kule kusulubishwa, yeye alisema, "Ndugu zangu, nilifanya bidii sana kuwaandikia habari za Imani iliyo yetu sote, kwamba mwishindanie Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja huko nyuma." Mnaona? Mnaona? Malaki alisema, kwa ajili ya siku za mwisho, yule nabii wa mwisho wa Agano la Kale, kwamba "Kabla haijaja ile Siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya, nitawapelekea Eliya nabii. Naye atairudisha Imani ya watoto iwarudie, ama Imani ya watoto iwarudie baba zao, kabla tu ya ule wakati wa maangamizi." Ni kitu gani? Ni Ujumbe unaotokea, Ujumbe na mjumbe wa siku za mwisho, ambaye hatawaleta kwenye kanuni za imani, bali atawanyakua kutoka kwenye kanuni hizo na kuwarudisha kwenye Imani ya asili ya baba zao, wale baba wa kipentekoste, ambapo Kanisa litakuwa katika siku za mwisho. Sio baba wa yaliyo ya Musa, bali baba wa kipentekoste.

177 Baba wa yaliyo ya Musa walikuwa ni Malaki 3, "Ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia mbele za Bwana." Mathayo 11:6 inasema jambo lile lile. Yesu anashuhudia ya kwamba hapo ndipo Yeye alipomwona Yohana, kasema, "Mlitoka kwenda kuona nini, mtu aliyevikwa ukosi mzuri, uliopinduliwa, na kadhalika? Siye Yohana." Yeye alisema, "Hao wanaovalia hivyo ni wa majumba ya mfalme, na madhehebu haya makubwa, ambao huwabusu watoto wachanga, na kufungisha ndoa, mwajua, na kadhalika, kuwazika wafu, na

kuwaoza vijana, na kadhalika. Wako huko nyuma." Kasema, "Mlitoka kwenda kuona nini? U—unyasi unaotikiswa na upepo wowote? La, si Yohana. La, la, yeye hakutikisika wakati walipolipuka dhidi yake."

178 Kasema, "Hutakuwa na ushirikiano wowote ukienda kule." Haikuleta tofauti yoyote kwa Yohana, alienda kwa vyovyote vile. Mnaona?

179 Kasema, "Mlitoka kwenda kuona nini, nabii?" Kasema, "Nasema, na zaidi ya nabii! Na kama mnaweza kulielewa, huyu ndiye aliyenenwa habari zake na nabii, akisema, 'Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia,'" Malaki 3.

180 Na katika Malaki 4, kwa ajili ya wakati wa kanisa, Yeye alisema, "Nitawapelekea Eliya kabla ya siku hiyo." Sasa, huyo asingeweza kuwa ni Yohana, maana ulimwengu haukuteketezwa huko nyuma wala wenye haki kutembea juu ya majivu ya waovu. La. Ni wakati huu, Ujumbe utakaotokea! Utakaofanya nini? Kuirudisha Imani ya hao watu, Kanisa siku hizi ambalo limetoka kwenye upotovu huu wote mbalimbali na mwili wa dhehebu, uliojaa vidonda na usaha, kuwarudisha kwenye Imani hai na Mungu aliye hai. Huo Ujumbe umekuwa ukiendelea kwa miaka kadhaa. Hiyo ni kweli. Ni wakati sasa ambao inatupasa kupokea na kuamini: uinjilisti wa wakati wa mwisho ni wa kurudisha. Yoeli alisema jambo lile lile, "Nitarejesha miaka yote iliyoliwa na parare."

181 Angalieni hapa. Mnaukumbuka ule Ujumbe wangu hivi majuzi juu ya ule mti wa Bibi-arusi, mnaona, jinsi walivyomchukua Yesu? Yeye alikuwa ni Mti, Ule ambao Daudi aliuona, Mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, tunda Lake katika majira yake, Mti ulio mkamilifu kuliko yote. Nao wakamkata na kumtundika juu ya mti wa Kirumi uliotengenezwa na mwanadamu, kwa ajili ya dhihaka. Lakini alifanya nini? Alifufuka tena kwenye siku ya tatu. Alifanya nini tena? Aliuweka Mti wa Bibi-arusi, mwanamume na mwanamke kama ile miti iliyokuwa katika bustani ya Edeni, miti miwili. Mmoja wao, mti wa uzima, na huo mwingine mti wa mauti. Naye alifanya nini? Alikuja kuukomboa mti huu. Kwa hiyo kwa kuwa Yeye aliukomboa, pale Kalvari, Yeye yuko tayari kuupanda sasa. Loo, jamani! Ninaanza kujisikia kubarikiwa unaposema hilo, unaona. Kuurudisha mti Wake wa Bibi-arusi, ule uliopaswa kuwa katika Edeni, bali ukaanguka kule kwa sababu haukuliamini Neno. Lakini hapa Yeye anaenda kuurudisha mti utakaoliamini Neno! Basi ulipotokea kwenye Siku ya Pentekoste, lile Fundisho la asili, ile Imani ya asili, basi Rumi ikaanza kufanya nini? Ikatuma parare, ikatuma tunutu. Na kila mmoja akaichukua sehemu yake kutoka kwenye hilo tunda, majani na kila kitu, wakaunyonya wote.

182 Lakini ni nini alichoona nabii ambacho, yeye alisema, "Lakini nitaurudisha mti huo, asema Bwana." Ulianza nyuma kwenye yale Matengenezo. Ulifanya nini? Uliunda madhehebu. Mungu akaupogoa, papo hapo katika Yohana Mtakatifu 14, akakatilia mbali dhehebu lote kutoka kwake. Nao ukarudi kwa Wesley, akaunda dhehebu. Ukapogolewa.

183 "Lakini nitarudisha!" Ungali unakuja. Sasa unafanya nini? Katika wakati wa jioni hakutakuwako na dhehebu. Kutakuwa na ki—kilele. Tunda huivia wapi kwanza? Kileleni. Kwa nini? Jua huligusa. Na katika wakati wa jioni mbegu zinapandwa sasa kwa ajili ya mti wa Bibi-arusi wa wakati wa jioni. Hapo Mti wa Uzima utakaporudi kwenye ule mti wa Bibi-arusi. Mwaona? Nazo Nuru za jioni zimetokeza sasa zipate kulitia maji na kuliivisha tunda ambalo limekuwa kwenye ule mti uliopandwa. Mbegu zimepandwa. Mnaona? Wakati wa jioni. Kwa hiyo uinjilisti wa wakati wa jioni utakuwa ndio alama ya Malaki 4, kuirudisha imani ya hao watu iirudie ile Imani ya baba zao. Naam, bwana. Moja kwa moja kwenye Mawe ya kujengea! Amina. Kurudi kwenye . . .

184 Leo hii viongozi tena wanasema, "Idadi, idadi!" Yale huko nyuma waliyosema katika siku za Yesu, kwenye kipindi hicho cha wakati. Yesu alisema "Enyi wanafiki! Enyi Waandishi, enyi Mafarisayo, ninyi mnazunguka bahari kufanya mtu mmoja kuwa mwongofu, kumpata mfuasi mmoja, ndipo mnapomwingiza ndani yeye ni mara mbili mtoto wa jehanamu kuliko wakati alipoanza." Na siku hizi wata—watatumia mabilioni ya dola na kufanya yote wawezayo kumfanya mtu mmoja zaidi mfuasi wa kanisa. Na, mnapofanya hivyo, yeye ni mbaya zaidi kuliko alivyokuwa huko nje. Mnaweza kumfanya tu mnafiki, kuwaacha watu wafanye mambo, watoke waende ulimwenguni na kucheka na kuidhihaki Injili, na kila kitu namna hiyo. Ni, mnaona, viongozi wa siku hizi tena wakisema, "Idadi, idadi, idadi!" Hilo, hilo tu ndilo linalojalisha siku hizi, ni idadi, kukata kauli.

185 Sasa, hilo ni neno kubwa sana leo hii, "kukata kauli." Laiti mtu angalikata kauli la kumtumikia Mungu badala ya kujiunga na kanisa. "Kata kauli, ingia ndani, weka jina lako kwenye kitabu," peleka umati mkubwa mno wa watu kule chini, wakajiandikishe. "Jina lako ni nani?" "John Jones." "Unamkubali Kristo kama Mwokozi wako?" "Naam." "Unamwamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu?" "Naam." Shetani anafanya jambo lilo hilo, jambo lilo hilo. Biblia ilisema alifanya. Yeye anaamini na kutetemeka. Naam, bwana.

186 Bali hutetemeki wakati kweli unaamini, unashangilia, amina: "Wote wanaopenda kuonekana Kwake." Kama nilivyosema mtu fulani sikuzote ananiambia, ananitumia barua, "Ndugu Branham, unawashtua watu nusura kufa, ukiwaambia mwisho unakuja." Ati kulishtusha Kanisa? Jamani, hilo ndilo jambo adhimu kuliko yote lingaliweza kutukia, Kuja kwa

Bwana, wakati wa mwisho. Laiti kungalikuwa ni sasa hivi. Hakika. Vema, ndilo jambo adhimu kuliko yote nililopata kuwazia, kumlaki Bwana wangu. Joho hili la kale la nyama nitaliangusha, kisha nifufuke na kuchukua tuzo la milele, kurudi kwenye ujana tena, na kuishi milele pamoja na Bwana wangu, pamoja na watu wangu wote. Mbona, jamani! Siwezi kuwazia kupambana na dhambi hii na majaribu, na maumivu na uchungu katika maskini nyumba hii ya wadudu hapa. Kukiacha kitu hiki na kuiendea ta—taji ya haki, mbona, ndilo jambo adhimu kuliko yote nililopata kusikia! Kama vile Mtume Paulo alivyosema, "Nimepiga vita vilivyo vizuri, nimeumaliza mwendo wangu, imani yangu nimeilinda, baada ya hayo kuna . . . Nimeilinda *ile* Imani, na baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana mwenye haki atanipa siku ile; si mimi tu, bali na watu wote wanaopenda kuonekana Kwake." Sio *wanaoamini* kuonekana Kwake; bali "wanaopenda" kuonekana Kwake, ni furaha kuu sana kujua Yeye yuaja! Bila shaka! Naam, bwana!

187 Lakini siku hizi ni "wafuasi," ni "kukata kauli," ni "waleteni wafuasi wa kanisa" wafuasi wengi sana. Hilo ndilo . . . Huo sio uinjilisti wa wakati wa jioni.

188 Sasa nitakoma kwa dakika moja tu, nami nataka tu kuwazungumzia kutoka moyoni mwangu. Ninatumaini sijaninii—sijawaweka muda mrefu kupita kiasi. Ni . . . nina yapata dakika saba, nane bado, nami ninataka tu kuwazungumzia kutoka moyoni mwangu.

189 Hiyo si ni kweli sasa, "Kukata kauli, jiunge na kanisa. Wewe liache kanisa la Methodisti uje ukajiunge nasi, la Kibaptisti. Ama, liache la Kibaptisti uje ukajiunge nasi, la Kimethodisti, Kipresbiteri, Kilutheri"? Katoliki inawachukua wote, mnaona. "Mfuasi, mfuasi, mfuasi, mfuasi, kukata kauli, kukata kauli."

190 Mawe yanafaa nini kama huna mwashi wa kuyachonga vizuri? Maungamo ni mawe. Wakati Petro alipofanya maungamo yake, Yesu alisema, "Wewe ni Petro, jiwe dogo." Lakini jiwe linafaa nini kama hakuna mwashi wa mawe pale wa kulichonga kuwa mwana wa Mungu? Unalundika tu lundo la mawe. Hiyo ni kweli? Hayafai kitu hata kidogo. Mnaona? Maji hulichakaza jiwe. Mnaona, hiyo ni kweli, hao ni watu. Mawe yanafaa nini kama huna mwashi wa mawe wa kweli aliye na chombo kizuri kikali kumchonga apate mahali pa kutoshea katika Nyumba ya Mungu? Ninataka tu kuwaulizeni, kukata kauli kunafaa nini, inafaa nini wewe kuliandika jina lako kwenye kitabu? Inafaa nini kuja kujiunga na kanisa, iwapo mwashi wa mawe hayumo mle atakayewachonga hao na kuwafanya waachane na *haya* na *yale,* na kuwakata na kuwafanya Hivi, na kuwaandaa kabisa na kuwafanya kama Wakristo waliowekwa katika Nyumba ya Mungu, wakiwa na ishara zinazowafuata waaminio?

191 Huo ndio uinjilisti wa wakati wa mwisho, kuyachukua mawe na kuyachonga. Mnaona?

192 Hayo mawe yangefaa nini kama ukiyalundika tu? Acha yakae mahali yalipo, huenda yakafanya kazi bora kidogo huko nje kuliko vile wangeyalundika pamoja. Huenda yakahitajika huko nje, na hakuna lolote huko nje. Mnaona, hiyo ni kweli. Jiwe halifai kitu pasipo na mwashi wa mawe.

193 Yesu huihesabu tabia, sio washiriki. Mnajua hilo? Yeye huihesabu tabia. Mungu daima amejaribu kumpata mtu mmoja mkononi Mwake. Hayo tu ndiyo Yeye anayohitaji, ni mtu mmoja, na Yeye ataifanya kazi Yake miaka yote. Wazieni tu, Yeye angeweza tu kumpata mtu mmoja mwenye haki katika siku za Nuhu. Katika siku za Musa, Yeye alimpata mtu mmoja tu mwenye haki.

194 Mwangalie Samsoni. Mnaona, Mungu anaweza tu kutumia kile unachosalimisha Kwake. Samsoni alikuwa ni mtu mkubwa mwenye nguvu, alikuwa na nguvu nyingi mno. Samsoni alimpa Mungu nguvu zake, bali asingempa moyo wake. Aliutoa moyo wake kwa Delila. Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo na watu siku hizi. Loo, ndugu, watajitolea na kulipa madeni, na mambo kama hayo, na kujenga dhehebu kubwa zaidi, na kadhalika namna hiyo, bali, inapofikia kutoa moyo wao, hawatafanya hivyo. Hiyo ni kweli. Inafaa nini . . .

195 Petro alikuwa na upanga. Aliuchomoa upanga huo, alikuwa akitaka kulikata sikio la kuhani mkuu, na vitu kama hivyo, akalikata. Lakini ilipofikia kwenye ujasiri halisi wa Kikristo, hakuwa nao. Alirudi nyuma na kumkana Yeye. Hiyo ni kweli? Angeweza kulikata sikio la kuhani mkuu kwa upanga wake, hakika, yeye alijua jinsi ya kuutumia. Bali ilipofikia kwenye ule mfinyo na wakati wa kulitetea Neno la Mungu, hakuwa na ule ujasiri, na hata akakana alimjua Yesu.

196 Hapo ndipo lilipo leo hii. Tunao ujasiri wa kujenga mijengo na kuweka mamilioni ya dola mle. Tunao ujasiri wa kuweka vinanda vya mabomba na viti vya anasa, na kila kitu, na kutoka nje na kuwaongoa watu kutoka mahali hadi pengine, na kuwafanya Methodisti wawe Baptisti, na kadhalika, huku na huku namna hiyo. Bali inapofikia kwenye ujasiri wa Kikristo, kulikubali Neno, Ujumbe wa Mungu, na kulitetea, sisi ni wachache. Kwa hiyo mawe yenu yanafaa nini bila mwashi wa mawe tena? Hiyo si ni kweli?

197 Mungu anaitafuta tabia, sio ufuasi. Tabia! Elieza, hapo alipoenda kumtafuta Bibi-arusi wa—wa—wa Isaka, alijitahidi mpaka akaipata tabia. Kumbukeni, Ibrahimu alimwajibisha kama vile Mungu anavyotuwajibisha, hiyo ni kweli, sisi wahudumu. "Kamtafute Bibi-arusi Wangu!" Mungu na aubariki moyo wako. Mimi siwatafuti wafuasi, ninawatafuta wenye moyo safi, mnaona, mtu fulani atakayeliamini Neno.

198 Elieza alitafuta, naye akawazia, "Loo, siwezi kufanya hivi mimi mwenyewe. Kuna wajibu mwingi sana. Ninatambua

wajibu wa kumtafutia Isaka . . . " Ambaye, ni mfano wa Kanisa, mwajua, Kristo; Rebeka, mfano wa Bibi-arusi. Naye Elieza alipiga magoti na kusema, "Mungu, Wewe—Wewe huna budi tu kunisaidia." Ndipo aliporejea kwa Mungu, Mungu alimsaidia. Akaipata tabia.

199 Rudi kwenye Neno, ndugu. Mrudie Mungu. Usilisikilize kanisa hili ulilo mfuasi wake. Unaweza kukaa mle ukitaka, kama watakuruhusu. Lakini, jambo la kufanya kwanza, ni, njoo kwa Mungu. Hiyo ni kweli. Huu ni uinjilisti wa wakati wa mwisho. Naam, bwana. Tabia!

200 Ndipo wakati alipogundua, na halafu wakati Elieza alipoipata ile tabia iliyokuwa ndani ya huyo mwanamke, Rebeka, yule bibi-arusi mrembo wa Isaka, yeye alimwambia kuhusu Isaka. Na yeye hakuuliza hata swali moja. Aliamini neno la yule mjumbe, kisha akajiandaa kwenda. Nao wakaenda, kamwuliza baba yake, yeye akasema, "Mwulize tu, huyu mjakazi ni mtu mzima. Mwulize, uamuzi wake umetosha."

201 Yeye akasema, "Nitakwenda." Kwa nani? Mwanamume ambaye hakuwa amewahi kumwona kamwe, hakujua lolote kumhusu. Lakini hata hivyo yeye alikuwa tayari, kwa sababu alichaguliwa tangu zamani na kukusudiwa kwa hilo. Kweli kabisa.

202 Mliona yule mwanamke aliyeitawadha miguu ya Yesu? Kamwe hakuomba baraka. Aliangalia tu pale. Na hapo, yule mnafiki akijaribu kumdhihaki, kuidunisha sifa Yake. Hivyo ndivyo sikuzote walivyokuwa wakijaribu kufanya, kumfanya aonekane duni. Watu wengine, mwajua, walimfuata wapate tu kufanya hilo. Wangesema, "Sasa, angalia hapa. Bwana Mwema, tunajua Wewe ni mtu mkuu wa Mungu, huogopi chochote. Inatupasa kutoa kodi kwa Kaisari?" Mnaona? Hayo mambo yote! Hayo, wakijaribu tu kupata kitu cha kulichafua Jina Lake, kulipaka tope. Naye Mfarisayo huyu akamwalika huko chini kwa chakula cha kutwa, hilo dhehebu likijua watamwalika huko, walikuwa na njama mahali fulani. Kama vile mpiga karata angalisema, "Alikuwa na mpango wa siri." Walikuwa na kitu kimoja shirika.

203 Unapomwona mtu yeyote kama huyo, anayekuchukia, unapomtetea Kristo, kisha wanakuingiza ndani, ama ni wapate fedha nyingi kutoka kwako, au wafanye jambo fulani, ama wakutumie kwa njia fulani. Unaona? Hakuna . . . Hawataamini Ujumbe. Wamekuleta pale kwa ajili ya jambo lingine. Mnafikiri Kristo yuyo huyo halitambui jambo lilo hilo siku hizi? Hakika, Yeye hutambua.

204 Bali walimleta mle ndani, nao wakasema, "Sasa tutalithibitisha." Nao wakamweka huko nyuma na kumwacha aje akinuka, kamwe hawakuitawadha miguu Yake, kamwe hawakumkaribisha. Ameketi huko kwenye lile, ambapo

wangetembea na majoho hayo, mwajua, kuleta hiyo ambapo farasi na kadhalika walikuwa wamepitia barabarani katika siku hizo, hivyo vijia vidogo. Wote wanasafiri vivyo hivyo. Joho hilo kubwa likiokota harufu mbaya, nayo ilikuwa juu Yake, nayo ilivunda kutokana na mavumbi na kadhalika barabarani. Na maskini huo mnuko, kama wa zizi na kadhalika. Nao huo ulikuwa juu Yake, akienda kwenye nyumba ya ugeni yenye yale mazulia makubwa makubwa ya sarara sakafuni, kila kitu. Walikuwa na namna fulani ya manukato, wali—walinawa uso wao na kutawadha miguu yao, kisha wakawapa jozi ya ndara za chumba cha kulala, kitu kama hicho, na kuweka makubadhi yao. Halafu akaingia akiisha kuvalishwa na kunadhifishwa, na kuchanuliwa nywele, kisha akaingia ndani. Ndipo unawalaki wageni wako, halafu basi—halafu basi—halafu basi—halafu basi unawasalimia na kuwakumbatia. Wanakumbatiana shingoni, na kubusiana shingoni. Mnaona? Kama mlivyoniona mimi na Joseph muda mfupi uliopita tukikumbatiana, tukipapasana. Basi walibusiana shingoni. Lakini Mfarisayo huyo, baada ya kumwalika Yeye mle ndani, naye Huyo hapo alikuwa ameketi pale nyuma, kamwe hawakuitawadha miguu Yake, hawakumfanyia chochote, walimwacha aketi pale wapate tu kumdhihaki.

205 Bali maskini mwanamke fulani kahaba mwenye sifa mbaya, akiwa na nikeli chache alizokuwa amepata huko nje katika maisha yake ya aibu, alimwona ameketi pale. Nayo machozi makubwa yakatiririka mashavuni mwake. Akashuka kule chini na kununua kibweta cha marhamu, kwa fedha zote alizokuwa nazo. Akanyemelea kwa njia fulani na kurudi pale, akaanguka miguuni Pake, akaanza kulia, nywele zake zikaanguka chini. Na—naye angelia na kuchukua ninii zake. . . Wao hawakuwa na taulo ya kuitawadha miguu Yake, naye alikuwa amezichukua nywele hizi na kuipangusa miguu Yake. Ni maji mazuri jinsi gani kwa ajili ya miguu Yake, machozi ya mwenye dhambi anayetubu! Na kama angaliusogeza tu mguu Wake, yeye angaliruka juu. Hakuwa akiomba chochote, aliona tu ilihitaji kufanywa.

206 Hivi hatuwezi kufanya hivyo siku hizi? Jamani, hatuombi chochote. Inahitaji kufanywa, Injili inapaswa kuhubiriwa. Kama tunapata senti, ama chochote kile, haileti tofauti yoyote. Sijawahi kuchukua sadaka maishani mwangu. Hii ni haja. Hii ni huduma. Umetengwa, na makanisa yanakuchukia, na kila kitu kingine, na kukurusha nje, na marafiki wachache tu unaowakusanya pamoja. Bali ni Ujumbe. Hauna budi kuenezwa, haidhuru. Kamwe mimi sikujiweka kwenye redio na vipindi vikubwa vya televisheni ambako ingenibidi kuwasihi watu wanipe pesa. Nisingeweza kufanya hivyo. Ninataka kuwa ndugu yenu. Ninataka kwenda ambako Mungu. . . Kama kuna watu watano hapa, niende kule. Niende huku, kama kuna milioni moja, Mungu atafanya njia kwa ajili yangu kwenda. Hivyo

tu. Kuliishi tu kwa imani. Hivyo ndivyo sote tunapaswa kuwa tukifanya. Na, Mungu ashukuriwe, wengi wao wanafanya hivyo, mnaona, vile vile. Hiyo ni kweli, wanafanya hivyo.

207 Mwangalieni maskini mwanamke huyu. Yesu kamwe hakuusogeza mguu. Mwangalieni maskini Mfarisayo huyu amesimama pale chini, kasema, akijaribu kumdhihaki sasa, kasema, "Sasa, kama alikuwa ni nabii, Yeye angejua ni mwanamke wa aina gani alikuwa akiitawadha miguu Yake. Mnaona? Angejua ni mwanamke wa aina gani aliyekuwa karibu na Yeye. Mnaona, Huyo hapo, hiyo inaonyesha tabaka analojishughulisha nalo." Nina furaha sana kwa ajili ya hilo. Naam. Yeye alijua. "Tazameni pale ni watu wa tabaka gani walio pamoja na Yeye. Sisi ni wenye vyeo. Sisi ni wafuasi wa kanisa. Basi, tazameni, maskini yule mwenye dhambi huko nje aliye pamoja na Yeye, mwanamke yule, tunajua ni nani, anazurura mitaani. Yeye ni . . ." Mnajua ninalozungumzia. "Kwa hiyo pale, alikuwa ni mwanamke wa aina hiyo. Angalieni, angalieni, hao ndio aina ya watu waliomfuata." Nina furaha sana. Nina furaha sana.

208 Hivyo ndivyo nilivyokuwa, mwajua. Nilikuwa watu wa aina hiyo, si mzuri, mwenye dhambi. Na kila mmoja wenu ni vivyo hivyo, ambaye hajamjia. Huji tu kusudi uwe mfuasi wa kanisa, unakuja kwa sababu kuna jambo la kufanywa. Yesu anahitaji kutumikiwa, mtu fulani anapaswa kuwa pale. Hebu na tulifanye. Kamwe hakusema, "Bwana, utanibariki, utafanya *hili*?" La, yeye aliitawadha tu miguu Yake na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake. Mwajua, baadhi ya dada zetu inawabidi kusimama kwa kichwa chao kupata nywele za kutosha kuipangusa miguu Yake.

209 Na hizo hapo nywele zake maridadi zilizojikunjakunja zimeanguka chini, naye akaipangusa miguu Yake. Huku "*busu*" alikuwa akiendelea kuibusu "busu" miguu Yake namna hiyo. Yesu aliketi tu na kumwangalia. Kamwe hakusogea hata inchi moja. Baada ya kitambo kidogo, alipomaliza, Yeye akageuka.

210 Huyo hapo maskini Simoni amesimama pale pamoja na shirika lote la wahudumu, kasema, "Mnaona! Ha! Ha! Huyo Ndiye. Mnaona, haya basi, hilo linaonyesha kile Yeye alicho. Yeye si nabii. Mwangalieni!"

211 Aligeuka na kusema, "Simoni!" Loo, ninawazia alikuwa mwekundu usoni. Akasema, "Nina jambo fulani la kukwambia. Ulinialika hapa. Unaona? Nilipoingia mlangoni, kamwe hukuitawadha miguu Yangu, kamwe hukunikaribisha kwa busu, kamwe hukunipaka mafuta kichwani. Ulisimama tu pale, ukijaribu kunidhihaki. Unaona? Ulinileta humu kwa kusudi hilo. Naye mwanamke huyu, tangu nilipokuja, tangu nilipokuja, ameendelea kuitawadha miguu Yangu kwa machozi yake, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake. Naye ameendelea, sio kuibusu shingo Yangu, bali kuibusu miguu Yangu."

"Hukutarajia chochote, sivyo, dada?"

"La."

212 "Lakini nakwambia kwamba dhambi zako, ambazo ni nyingi, zote zimesamehewa." A-ha. Naam. Mnaona? Kote kote yeye hakuwa na kitu hata kidogo, ila hofu tu kwamba hakuwa akifanya jambo jema, labda, lakini lilihitaji kufanywa, bali thawabu yake ilikuja mwishoni.

213 Huenda ukanisikia nikiuhubiri Ujumbe huu. Huenda ukamwona Roho Mtakatifu akitambua na kufanya mambo makuu, na kufanya miujiza. Huenda ukaomba, na lisitimie. Endelea, thawabu yako inakuja mwishoni. Hilo si lingekuwa ni bora zaidi papo hapo? Naam. Unaona, mtumikie Yesu. Huo ndio Ujumbe wa wakati wa mwisho. Yeye alikuwa na Bibi-arusi. Mungu anatafuta tabia. Ndipo basi Elieza akiisha kuipata ile tabia, basi jambo lililofuata lilikuwa ni kumwandaa kwenda. Hilo ni jambo lile lile sasa, ndugu, lile lile sasa. Ujumbe wa wakati wa mwisho hauko huko nje katika Babeli.

214 Hapo ndipo nilipokwambia, Joseph, wakati maskini huyu ndugu yangu Mswidi aliposimama pale nje na kuweka kichwa chake begani mwangu siku moja na kulia kama mtoto mchanga. Akasema, "Ndugu Branham, Mungu alinituma hapa, Chicago, akasema nitaona Chicago ikitikiswa moja ya siku hizi." Kisha akasema, "Sasa wananifukuza. Wanaliondoa kanisa langu moja kwa moja chini yangu, kanisa kuu, lililo zuri kuliko yote Chicago." Kasema, "Wanalichukua kanisa langu, nao hapa wamenifanyia mapinduzi. Walinitoa kwa kura. Sijui la kufanya."

215 Nikamwambia, "Joseph, Mungu hasemi uongo." Nikasema, "Umeona Chicago ikitikiswa. Hiyo ilianza katika Jiji la New York nilipokuona huko, kwa kuwa wasingeshirikiana nawe, hata nisingeenda." Wala hata sikumjua, bali kitu fulani kumhusu kilichonivutia kwake. Sisemi hili maana mkutano wake wa kimishenari ni usiku wa leo. Lakini, hiyo ilikuwa ni kweli, nilivutiwa na Joseph. Nilikataa kwenda Chicago, kwa sababu wasingemruhusu kuja, wasingemruhusu kuingia katika ushirikiano. Nikasema, "Basi nami siendi pia."

Kasema, "Wewe humfahamu."

216 Nikasema, "Ninajua simfahamu, bali Mungu anamfahamu. Yeye ni mtumishi wa Mungu. Na, kwangu mimi, yeye yuko sawa."

Na kwa hiyo basi Joseph akasema, "Laiti ningaliiona Chicago ikitikiswa."

217 Loo, jamani! Kutotambua kutikiswa kwake hakumaanishi chakula kile cha mzinga huko nje. Haimaanishi takataka ile itakayoangamizwa huko nje. Kanisa linatikisika. Mnaona? Kulikuwako tu na mia moja na ishirini kutoka kwa mamilioni,

kwenye chumba cha juu, wakati kule kutikiswa kulipokuja. Hiyo ni kweli. Hakika. Linatikiswa, ni wale watu. Ninii . . .

218 Tazameni, wakati walipokuwa na ule uamsho mkuu, huyu Apolo, yule mhubiri wa Kibaptisti ambaye hakuwa amempokea Roho Mtakatifu bado, kamwe hakuwa amebatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Paulo anapitia nyanda za juu za Efeso, anakutana na kanisa hili kuu Biblia inalonena habari zake, basi akaenda kule na kuwaambia njia ya Bwana. Nao wakasema . . . Akasema, "Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?" Nao walikuwa wakipiga makelele na kuwa na wakati mzuri sana. Kasema, "Mmempokea Roho Mtakatifu?"

Kasema, "Hatujui kama yupo."

Kasema, "Basi mlibatizwaje?"

Wakasema, "Tumebatizwa chini ya Yohana."

219 Akasema, "Huo haufanyi kazi tena. Hamna budi kubatizwa tena." Ndipo akawabatiza tena, katika Jina la Yesu Kristo. Naye akaweka mikono yake juu yao, ndipo Roho Mtakatifu akawashukia. Wakanena kwa lugha na kutabiri. Na walikuwako tu wanane ama kumi. Hiyo ni kweli.

220 Kutikiswa! Mnaona, Mungu hawatikisi hao, kuzimu itawatikisa wakati itakapowapokea. Bali Mungu hulitikisa Kanisa Lake.

221 Malaika mmoja aliwajia Ibrahimu na kundi lake mlimani, akafanya mwujiza, kwa kuyatambua mawazo yaliyokuwa moyoni mwake. Hiyo ni kweli? Naye Sara akiwa ndani. Ambapo, wale malaika walioenda Sodoma walikuwa na maelfu kule chini. Mnaona, kutikiswa huja kwenye kundi dogo. Umekuona, Joseph. Umeiona Chicago ikipata wito wake wa mwisho. Hiyo ni kweli. Naye Mungu alikuheshimu, akafanya vile hasa Yeye alivyosema. Kumtayarisha Bibi-arusi, hivyo ndivyo ilivyo.

222 Sasa tutamalizia papa hapa, kwa kusema hivi. Ujumbe wa wakati wa mwisho ni wa kumfanya tayari Bibi-arusi na kumwandaa kwa ajili ya Kunyakuliwa. Unaweza kufanya nini? Kulingana na Malaki 4, ni kuwarudisha kwenye ile Imani iliyokabidhiwa watakatifu mara moja. Kuwarudisha kwenye Imani ya baba zao, ile sehemu ya kipentekoste, katika wakati wa kurudishwa. "Nitarudisha, asema Bwana." Hilo ndilo tukio halisi, uinjilisti wa wakati wa mwisho.

223 Sasa ninataka tu kusema maneno haya machache kabla ya kufunga. Niliyapita Maandiko hayo mengine, na labda wakati mwingine ninaweza kuyarudia. Lakini ninataka kusema hivi. Tunaamini tuko katika wakati wa mwisho. Tunaamini hilo. Na ingawa inaonekana kama kwenye wakati wa mwisho, wakati huu, kwamba Ujumbe na Mjumbe wote wawili karibu wamevunjika-vunjika. Inaonekana kana kwamba Shetani amejaribu kadiri awezavyo kutuangamiza. Ndugu Neville,

ajali yake; Ndugu Crase pale; na bunduki kuilipua. Mnaona, inaonekana hivyo, na sasa hivi wakati kila kanisa kote huko nje limenikataa. Na, mnaona, mnaona, inaokekana kama ni—karibu umevunjika. Inaonekana kana kwamba tumeshindwa. Msiwe na wasiwasi. Mwajua, kwa kawaida ni kwenye wakati huo ambapo Mungu huingia jukwaani, kwa kitu ambacho amekuwa akikiangalia kwa muda mrefu. Ninyi kumbukeni.

224 Anakumbuka wakati mmoja kulikuwako na watoto fulani huko chini katika tanuru la moto, walikuwa wamelishikilia Neno kwa kweli. Kila kitu kikaenda kombo. Wakawatupa gerezani. Wakawaweka usiku kucha, walikuwa wawateketeze kesho yake asubuhi. Basi ilionekana kana kwamba mwisho ulikuwa umekaribia, walikuwa wakienda moja kwa moja kwenye lile tanuru. Lakini alishuka akiendesha apate kubadilisha, mandhari hayo yalibadilishwa katika dakika moja.

225 Daima ni katika nyakati hizo dhaifu mno, wakati inapoonekana kana kwamba Ujumbe wa kweli karibu umeshindwa, hapo ndipo Mungu anapoingia. Yeye—Yeye huuacha Ujumbe pamoja na mjumbe wafike mwisho wa safari yao, unaona, ndipo Yeye anaingia na kuyaabiri yale mawimbi makubwa. Hiyo ni kweli.

226 Kumbukeni, ilikuwa ni Yesu, wakati adui Zake walipofikiri wamemshinda, asiyeamini akasema, "Tumemweka msalabani." Masadukayo na Mafarisayo waliomchukia na kumtundika msalabani, wao waliwaza, "Tumempata sasa." A-ha. Ilikuwa ni yapata wakati huo ambapo Mungu aliingia jukwaani, akamfufua kwenye asubuhi ya Pasaka, na kuzivunja falme za Shetani, akaifagia kuzimu, akachukua funguo za mauti na kuzimu, kisha akafufuka pamoja nao. Hakika, ilikuwa tu kwenye wakati huo dhaifu. Ujumbe Wake, Yeye alikuwa amelihubiri Neno, alikuwa amelitetea, na kila kitu, basi ulikuwa ni wakati huo ulio dhaifu sana ambapo ushindi ulikuja. Wakati alipofanya yote aliyoweza kufanya, ndipo Mungu akaingia. Aliyabadilisha mandhari.

227 Ilikuwa ni Yakobo akimtoroka Esau, akikwepa *hapa* na *pale* (hata kwenye...?..., na wengine mbalimbali) katika kujaribu kujificha kutoka kwa Esau. Ndipo moyo wake ukaanza kutamani kwenda nyumbani. Basi akienda zake nyumbani, aliwatuma wajumbe, akatuma matoleo na kila kitu kingine, akijaribu kumtuliza Esau. Lakini ilikuwa ni wakati Yakobo alipofika mwisho wake, ilikuwa ni wakati Yakobo hakujua ageukie wapi. Alimvusha mke wake na watoto ma—majini, kisha akavuka ki—kile kijito. Ilikuwa ni wakati Yakobo alikuwa amepiga mwereka usiku kucha, mpaka nguvu zake zikaisha, naye akalemaa na alikuwa dhaifu, nao mwili wake ulikuwa umevunjika. Ilikuwa ni kwenye wakati huo ambapo Mungu alishuka akaingia jukwaani. Kesho yake asubuhi, tunamwona vipi? Mtawala shupavu, baada ya udhaifu wake. Ilionekana

kana kwamba alikuwa ameshindwa. Lakini tunamwona akiwa mtawala shupavu. Ujumbe ulikuwa ukiendelea, naye mjumbe alikuwa pamoja nao. Hiyo ni kweli kabisa. Alikuwa mtawala shupavu majuzi.

228 Esau, hata, wakati alipomhitaji sana, Esau, wakati alipokutana naye. Pia kumbukeni, wakati uo huo wote Mungu alitenda kazi katika moyo wa ndugu yake, pia. Hiyo ni kweli. Naye Esau akamjia, kasema, "Ninayo majeshi hapa." Kasema, "Ah, wewe ni dhaifu, Yakobo. Mwili wako umeteseka. Umevunjika." Kasema, "Ni—ni—ni . . . nitakutumia askari wakulinde," wakati hasa alipowahitaji.

229 Bali alikuwa amepata kitu fulani. Kasema, "Nitaenda peke yangu." Amina. Ni wakati alipopona kutokana na ule udhaifu, alikuwa amepona kutokana na ule mshtuko.

230 Wakati Yesu alipokuwa amepona kutokana na mshtuko wa mauti, Yeye alikuwa na nguvu kuliko wote, Yeye angeweza kupitia jengoni pasipo kuondoa saruji ya jiwe. Angeweza kula samaki na mkate. Amina. Loo, naam. Ilikuwa ni wakati huo, baada ya udhaifu kuja, ambapo alijikuta akiwa na nguvu. Ilikuwa ni baada ya udhaifu kuja.

231 Basi inaonekana ni dhaifu sana sasa kwa Ujumbe na mjumbe pia. Lakini msiwe na wasiwasi! Mahali fulani, sijui ni jinsi gani, bali ninamtumainia Yeye. Atakuja akiendesha jukwaani siku moja. Msiwe na wasiwasi. Hebu twendeni pamoja. Hebu tuinamishe ninii vyetu—hebu tuinamishe vichwa vyetu pamoja. Uinjilisti wa wakati wa mwisho.

232 Ee Mungu, zile Nuru kuu za jioni zimekuwa zikiangaza kwa muda fulani sasa. Tumekuona Wewe ukipitia kwenye marefu haya ya kanisa hapa, ukiwaleta wale waliokuwa ni vivuli tu vya wanaume na wanawake, wameliwa na kansa, vipofu, wagonjwa na wanaoteseka, madaktari kutoka hata kutoka Mayo na kila mahali wamewakatia tamaa. Sasa wameketi hapa asubuhi ya leo, na wengi wao wenye afya na nguvu. Sio hapa tu, bali kote ulimwenguni. Wanawake waliwapokea watoto wao waliofufuliwa, wakiisha kufa kwa saa kadhaa. Watoto wakiuawa barabarani, kwa magari, wakatangazwa "wamekufa" na kulazwa nje, hamna mfupa mzima ndani yao; na katika dakika moja wanatembea barabarani, wakimsifu Mungu. Naam, Bwana, Wewe ni Mungu. Wakati wa jioni upo hapa. Mbegu za kiinjilisti za jioni zimepandwa, Baba, na sasa inaonekana kana kwamba kidogo inaingia wakati wa kulemazwa. Wengi wa hawa . . .

233 Wakati ulipojitokeza jukwaani kwa mara ya kwanza huko nyuma katika kipindi Chako cha wakati, wote, "Nabii yule kijana wa Galilaya!" Loo, wote walikuzunguka. Bali ulipoanza kuwagonga na kuwaambia juu ya kanuni zao za imani na—na kadhalika, basi walikuacha. Ilikubidi kusimama peke yako.

Na hatimaye wakakupeleka Kalvari. Ilionekana kana kwamba walikuwa wameshinda, ilionekana kana kwamba kundi la—lao kuu la kiakili lilikuwa limelishinda kusudi la Mungu. Lakini, loo, hapana! Kwenye asubuhi ya Pasaka dunia ilikuwa na baridi ya wasiwasi, kaburi likafunguka naye Mwana wa Mungu akafufuka. Yeye alikuwa na funguo za mauti na kuzimu. Yeye alikuwa na haki ya kutoa ubatizo wa Roho Mtakatifu basi. Akaliambia Kanisa Lake, "Pandeni kule Yerusalemu mkangojee, nami nitamtuma juu yenu, kisha mtanishuhudia Mimi hata nitakaporudi tena."

234 Ndipo basi ukasimama na kuwaambia jinsi wakati utakavyokuwa, nasi hawa hapa katika wakati wa mwisho. Bwana, njoo ukiendesha tena, sivyo, Baba? Tunachoka, tumedhoofika. Mwanadamu ametukatalia kutoka kila mahali, madhehebu yote yametukataa. Huko California, hao watakatifu wa thamani wakisimama huko na kulia, makanisa arobaini, naye kiongozi huyo mmoja akasimama na kusema, "Vema, ikiwa yeye hubatiza, akitumia Jina la Bwana Yesu, hatumtaki." Naye akawakatalia Injili maskini watu hao wenye njaa.

235 Basi, Baba, nikasema, "Njoo unikabili kwa Maandiko," wala asingefanya hivyo. Kwa nini? Yeye anafahamu vizuri zaidi. Baba, mbona—mbona mataifa wamefanya ghasia nao makabila wakatafakari ubatili? Kweli kwa kuunyosha mkono wa Mwana Wako Mtakatifu Yesu, kuwaponya wagonjwa, na kuonyesha ishara na maajabu ya wakati wa mwisho. Limejirudia, Bwana. Ninawaombea. Mungu, usiwaache wakatupwe nje. Wengi wao ni watu wazuri mle ndani bado. Lijalie, Bwana, kwamba wataliona na kutoka.

236 Na maskini kusanyiko letu asubuhi ya leo, Baba, hatuijui mioyo ya hawa watu. Wewe unaijua. Kundi hili dogo hapa. Ninatoka moja kwa moja huko, kwa vyovyote vile. Na sasa kabla hatujaondoka kanisani, Bwana, kundi hili dogo linalokaa hapa, wao ni wasafiri. Hawakiri kuwa wa ulimwengu huu, Bwana. Wao ni wageni. Wamezaliwa mara ya pili, wao ni viumbe vipya. Wametoka kwenye mambo ya ulimwengu, kumtumikia Mungu, wakijua ya kwamba, "Hatuutamani utajiri wa ulimwengu huu ambao unaoza upesi sana. Tumeyajenga matumaini yetu juu ya mambo ya Milele, hayatapita kamwe."

237 Baba wa Mbinguni, kama kwa bahati kungekuwako na mmoja au zaidi miongoni mwetu asubuhi ya leo ambaye kamwe hajawahi kuhisi kwamba wanapaswa kupiga hiyo kona, naomba kwamba utanena na mioyo yao wakati huu. Basi jalia kwa utamu na unyenyekevu, mioyoni mwao, wayasalimishe tu yote Kwako, na kusema, "Bwana Yesu, unirehemu, mwenye dhambi. Sitaki kufa katika hali hii niliyo nayo sasa. Na bila kujua hata kwamba nitaishi siku nzima, basi si ni ujinga kupoteza muda wangu juu ya mambo ya kilimwengu!" Na kila kitu hapa kitaangamia, nao watu wataangamia pamoja na ulimwengu. Lakini Mungu, Baba

wa Milele, hawezi kuangamia, wala watu Wake. Jalia walikubali sasa, Baba yetu wa Mbinguni.

238 Zitakase leso hizi zilizowekwa hapa kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka. Walisema walichukua kutoka kwa mwili wa Paulo, leso na nguo, pepo wachafu wakawatoka. Waponye wagonjwa walio miongoni mwetu asubuhi ya leo. Naomba kwamba hapatakuwapo na mtu mnyonge miongoni mwetu.

239 Jalia Roho Mtakatifu mkuu atembee kwenye kusanyiko hili sasa, na ujalie kila mtu autambue Uwepo Wake. Na kama vile nilivyonukuu hapo mwanzoni, wakati dhoruba inapokuja katika msimu mkavu wa kiangazi, upepo umekuwa ukichoma na ni joto, mavumbi yamekuwa yakivuma, lakini, mara moja, tunaweza kusikia ngurumo, tunaweza kuona mawingu yakipanda. Nami nilisema ile ishara nyekundu imeshushwa, Yeye yuaja. Nasi tunahisi upepo mwanana baridi, kukaribishwa kwa Roho Mtakatifu wakati Yeye akipitia sehemu zetu zilizokauka. Tusaidie leo hii. Waokoe waliopotea. Jaza kwa Roho Mtakatifu, Bwana, upesi, kabla taa hazijazima, kwa kuwa ile ishara imeshushwa tayari. Maskini ile meli ya kale ya Sayuni imo jengoni sasa, na haitachukua muda mrefu kabla haijaanza kuita. Na, mara, watatoa gazeti, "Ni kitu gani kilichotukia? Mamia ya watu kote nchini wametoweka."

240 Ee Mungu, basi imechelewa kupindukia kwa hao wengine, Unyakuo umekuja. Hukumu itaipiga dunia, wenye haki wataondoka. Ndipo wataenda makaburini, na kusema, "Vema, hivi...Kwani walililifungua kaburi hili? Vema, imekuwaje hapa?" Loo, yule aliyemtumaini Mungu, aliyekufa miaka mingi iliyopita, atakuwa amekwisha kuondoka. "Ndipo, loo, ni kilio na maombolezo ya jinsi gani wakati waliopotea watakapoambiwa mwisho wao. Watailillia miamba na mlima," kulingana na Maandiko, "wataomba, bali maombi yamechelewa kupita kiasi." Jalia isiwe hivyo kwa wowote waliopo hapa leo hii.

241 Basi wakati tumeinamisha vichwa vyetu, mioyo yetu imeinamishwa, pia. Mimi ni mtu wa kipekee sana kuhusu kuwaalika watu madhabahuni, ninaamini si fundisho la kimitume. Ninaamini papo hapo unapoketi unafanya uamuzi wako, kama kweli unataka kuishi ama kufa. Ninaamini ni juu yako. Na kama kuna mtu hapa ambaye kamwe hapo awali kweli hakuliona tu jinsi hiyo, na kutambua saa tunayoishi, na ungenitaka tu nikukumbuke katika maombi, kwamba unataka kuwa Mkristo, nawe unataka kuwa kama Kristo maishani mwako na kuwa tayari kwa ajili ya kuja Kwake, mnaweza kuinua tu mikono yenu kote jengoni. Bwana akubariki, na akubariki, na akubariki, na wewe, na wewe. Mungu akubariki huko nyuma, akubariki huku chini. Hilo ni jema. Mungu akubariki, ewe msichana, moja kwa moja katika njia panda za maisha, dada. Huo ni uamuzi mkuu. Huenda umefanya ninii nyingi kuu...Mungu akubariki, baba. Naam, huenda

umefanya kazi siku nyingi ngumu maishani mwako, pia, na kumlea mtoto mdogo. Mama, wewe unayeketi karibu naye. Ee Mungu! Labda umeilea familia yako na kufanya mambo mengi makuu, ukayapapasa mashavu ya huyo mtoto mchanga wakati alipokuwa akilia, ukakipembeza kitanda kwa maskini mikono yako michanga, sasa imezeeka na ni dhaifu. Huenda ulimpembeza mtoto mchanga na kufanya mambo mengi mema, lakini jambo jema kuliko yote ulilopata kufanya lilikuwa ni wakati ulipouinua mkono wako wakati huo. Yeye alikuona. Samahani, tafadhalini.

242 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe umeiona hiyo mikono. Unajua kilichokuwa nyuma yake. Sasa wao ni kumbukumbu za mkutano huu. Ni kumbukumbu za Ujumbe. Wewe ulisema, "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, wala hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Nawe ulinena na watu hawa. Nao walikuwa wameketi pale, na kulingana na sayansi wasingeweza. . .mikono yao inapaswa kubaki chini, maana nguvu za uvutano zinaishikilia chini. Lakini walivunja na kuasi kanuni za sayansi. Wana Roho ndani yao iliyouinua huo mkono, ambayo ni kinyume na sayansi, kwa sababu Roho humo ndani anaweza kuivunja sayansi. Nao waliinua mkono wao kwa sababu kulikuwako na Roho wa Mungu aliyewazunguka, aliyesema, "Wewe ni. . . wewe unamhitaji Kristo." Ndipo wakainua mikono yao juu, "Nikumbuke, Ee Bwana."

243 Kama yule mwizi aliyekuwa akifa msalabani, kasema, "Unikumbuke utakapokuja katika Ufalme Wako."

244 Na Wewe ulimwambiaje? "Leo utakuwa pamoja na Mimi Paradiso."

245 Nami naomba, Baba, ya kwamba siku ii hii kwamba utawachukua katika Ufalme Wako, katika ushirika Wako hapa duniani, kila mmoja wa hawa waaminio, na uwafadhili. Yesu, Wewe ulisema, ulipokuwa hapa duniani, katika Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamni Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele; wala hataingia hukumuni, hawatakuwako wakati hukumu itakapoipiga dunia, bali wamepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Uliliahidi jambo hilo, Bwana. Ninawadai. Na sasa kwa wote walioinua mikono yao, na hata wale ambao moyoni mwao waliamini ya kwamba wanapaswa kuinua, na hawakuinua, ninawakabidhi Kwako asubuhi ya leo, Baba, kama kumbukumbu za rehema za Yesu Kristo na za Neno Lake ambalo tumelihubiri asubuhi ya leo. Wao ni Wako. Waweke salama, Bwana, mpaka siku ile. Na jalia wakue kama watoto wachanga. Jalia maji hapa kwenye kidimbwi yawapate, kwa kuwa wamekiri dhambi zao, wamekufa, wakazikwa katika Kristo, wapate kufufuka tena kwenye uhai mpya, wakatembee katika ulimwengu mpya, watembee na marafiki wapya, watembee katika kundi jipya,

watembee na malaika, watembee katika Uwepo wa mambo ya Kimbinguni. Mambo hayo ambayo hawawezi kuyaona yaliyowazunguka, bali wanahisi na kujua kwamba yapo. Hayo ndiyo mambo yadumuyo, mambo ya Kimbinguni ndiyo yadumuyo. Tunawakabidhi Kwako Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

246 Sasa, nasikitika nimewakalisha kidogo kupita wakati, nami nina hakika ya kwamba nyinyi. . . Mnajisikia vizuri? Sasa, mkutano, wakati mwingine inanibidi kakata na kufinya. Sasa kwenu mlioinua mikono yenu na mnamwamini Bwana Yesu, watakuwa na ibada ya ubatizo, nadhani, jioni ya leo. Ama, naam, nafikiri vidimbwi vimejazwa kama mkiutaka sasa hivi, na majoho na kadhalika yako tayari. Ukitaka kubatizwa sasa hivi, wakati wowote, tupo tu hapa kufanya hilo. Na sasa baada ya kukatakata na kupasua. . .

247 Tu—tunawashukuru ninyi wageni malangoni petu, kuja na kushiriki pamoja nasi asubuhi ya leo kwenye Neno la Mungu, tunakuthamini kuja kwenu. Bwana awabariki. Tuna furaha sana mlikuwa hapa.

248 Ninamwona rafiki yangu ameketi nyuma ya jengo hapa, sijamwona kwa muda mrefu. Hata sijui jina la huyu mvulana. Yeye ni rafiki yangu mwema. Yeye ni binamu wa msichana niliyekuwa nikiambatana naye, Marie Francisco. Siwezi kukumbuka ni nani wala jina lake ni lipi. Waweza kuinua mkono wako? Tuna furaha kuwa nawe umekeketi hapo na Mungu akubariki. Mvulana huyo amekuwa Mkristo kwa miaka mingi. Nami. . .

249 Rafiki yangu hapa, Jim Poole, ni wangapi wamepata kunisikia nikimtaja Jim Poole, rafiki wa ujanani, mwanawe na mkewe.

250 Pia Donny, siwezi kulikumbuka jina lake la mwisho. Gard—Gard, Donny Gard na maskini mke wake mpendwa hapa. Walikuwa huku nyumbani jana kunitembelea. Nafurahi sana kuwa nao asubuhi ya leo.

251 Nami ninaamini huyu ni ndugu mgeni anayeketi papa hapa karibu na Ndugu Way. Na, loo, kwa hiyo, papa hapa, labda nimekosea, na wakati mwingine mimi husahau nyuso. Nami nina furaha kuwa nanyi nyote hapa ndani asubuhi ya leo.

252 Na sasa, kabla hatujaondoka, baada ya kukatakata. . . Na, mwajua, Biblia ilisema Neno la Mungu. . . kama uamuzi ule, kufanya jiwe, bali inakubidi kuwa na mkata mawe apate kulikata hilo kabisa, na kufanya sura yake. Mnaona? Na Waebrania mlango wa 4 ilisema, "Neno la Mungu ni kali na lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili." Linakata, linatahirisha, linakatilia mbali ya ziada. "Hata huyatambua mawazo na makusudi ya moyo," Neno la Mungu. Nalo hukata.

253 Sasa, kwa ajili tu ya kuabudu, hebu tuimbe tu maskini wimbo mdogo wa kale niupendao, mmoja wa zile nizipendazo, "Nampenda, nampenda." Ni wangapi wanaompenda kweli? Sijali kama wewe ni Mkristo ama la, wewe sema "Nampenda kwani Yeye alinipenda kwanza." Hebu tuuimbe pamoja sasa, sote pamoja.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

254 Hivi hamuupendi huo? Hebu tuuimbe tena. Mnapofanya hivyo, peaneni mikono na mtu fulani aliye karibu nawe. Usisimame, sema tu, "Mungu akubariki, ndugu," mtu aliye karibu nawe, kusudi wewe, kila mtu ajisikie kukaribishwa kabisa. Hayo ndiyo makaribisho yetu hapa maskanini, kutoka kwangu, kila mmoja wenu. Vema.

Nampenda, nampenda

Mungu akubariki, ndugu.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

255 Na tuviinamishe vichwa vyetu tunapouvumisha. Sasa mnyoshee mkono wako, kwa urahisi sana. Sasa, Yeye si ni wa ajabu? Naam.

256 [Ndugu mmoja ananena kwa lugha nyingine. Ndugu Branham anatulia—Mh.] Iweni tu na kicho kabisa kwa muda mfupi.

Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Watanena kwa lugha mpya. Wakishika nyoka au kunywa kitu cha kufisha, hakipaswi kuwadhuru, kwa ajali ama kulipuka hakitawadhuru. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

Ngojeni tu kidogo, tuone kama fasiri itatokea kwa ajili ya huu. Kama wageni wamo malangoni mwetu, tunangojea kuona yale Bwana atatwambia kupitia kwa ujumbe huu.

[Ndugu fulani anatafsiri—Mh.] Tafsiri. Amina. Hiyo ndiyo tafsiri ya yale mtu huyu aliyosema. Kwa wale watu hapa ambao huenda wasijue ni kitu gani, ni Roho. Inatendeka mara kwa mara maskanini, kutoa ujumbe kwa watu.

Na tuombe.

257 Baba wa Mbinguni, tunakushukuru kwa ajili ya hili, bila kujua kwamba mtu fulani mahali fulani, ya kwamba Wewe ulisema na moyo mmoja mahali fulani nao ukajibu tena, hata katika ujumbe wa kumalizia, Yeye alisema, akawaita "watoto" Wako, kwa sababu Wewe ulikuwa umewaita, na labda walikuwa wakijitayarisha kuondoka pasipo kukupokea Wewe. Huu, huu

ujumbe umekuja tena. Kwa hiyo tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utajalia sehemu kubwa ya Roho Wako juu ya mtu yeyote huyo. Kamwe hukulitaja jina lao, Wewe ulinena tu. Na kwa hiyo, Baba, labda hivyo ndivyo unavyolitaka. Nasi tunaomba tu, Baba, ya kwamba mapenzi Yako yajaliwe mtu huyu ama watu hawa, wowote wale, ambao labda wanashuka kuja kwenye wito wa mwisho. Ninaomba, Baba, ya kwamba sivyo, bali, asubuhi ya leo kama watampokea na kuamini kwa moyo wao wote, wakiisha kuusikia Ujumbe kama vile Wewe umenena na kusema, kisha jalia waupokee kwa kikombe kilichoinuliwa, kumpokea Roho. Jalia wasimame na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zao, na kwa utamu wajazwe na Roho Mtakatifu, na kuongozwa katika maisha ya utumishi na furaha. Ninalikabidhi Kwako sasa, Baba, na kusanyiko, katika Jina la Yesu. Amina.

258 Jumbe hizo wakati mwingine hunena, mtu fulani, hatujui ni akina nani. Wakati mwingine zinasema kwamba ni nani, bali mtu fulani hapa tu ambaye huenda alianza tu kuondoka bila Yeye. Na wakati unapofanya hivyo, kumbuka, huyo ni Roho Mtakatifu akinena kwa lugha fulani hata inahitaji tu uvuvio; yeye yule aliyeinena, yuyo huyo huifasiri. Sasa, kumbukeni yale ndiyo kwanza nimalize kusoma, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Mnaona, hiyo ni miongoni mwa waaminio. Hatuamini ya kwamba inawapasa watu wote kufanya hivyo. Tunaamini ya kwamba hushuka kanisani miongoni mwa watu. Wakati mwingine watu huja hapa, hawajawahi kusikia kitu kama hicho awali, naye Roho Mtakatifu anawashukia na kutoa ujumbe, na kuwaponya watu wanaoketi hapo wakifa kwa kansa, na kila namna ya magonjwa na kadhalika, wanarudi moja kwa moja tena. Ni Roho Mtakatifu miongoni mwa watu Wake.

259 Mnampenda? Amina. Ninampenda, pia. Tunatumaini kuwaona usiku wa leo. Na sasa Ndugu Neville, nitarudisha ibada kwa Ndugu Neville, mchungaji wetu. Vema.

62-0603 Uinjilisti Wa Wakati Wa Mwisho
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org